**KITABU** cha IGP Mwema chageuzwa darasa la polisi

UKURASA 3



**KERO** za wananchi zaishtua CCM, yawaita mawaziri kutoa ufumbuzi

UKURASA 2


Nipashe Spotika

VIUNGO WA4 WANAOWEZA KUWA SAHIHI PALE ARSENAL

ISIKUPITE

UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatatu Juni 26, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0581353

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Mwanasheria achambua kifungu kwa kifungu mkataba wa Bandari


INTERGOVERNMENTAL AGREEMENT

BETWEEN

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

AND

THE EMIRATE OF DUBAI

CONCERNING

ECONOMIC AND SOCIAL PARTNERSHIP FOR THE DEVELOPMENT AND IMPROVING PERFORMANCE OF SEA AND LAKE PORTS IN TANZANIA

**AFAFANUA** ukomo wa mkataba, usuluhishi Afrika Kusini. Ndugai naye atangaza msimamo wake... *Endelea ukurasa wa 2 & 4*



Rais Samia Suluhu Hassan akisikiliza maelezo ya wataalamu kwenye banda la maonyesho la Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), kuhusu kazi inazozifanya wakati wa maadhimisho ya kupiga vita matumizi na biashara ya dawa za kulevya duniani katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Samia aagiza waraibu dawa za kulevya kupewa mikopo ya 10%

UKURASA 2

UKURASA WA 8

## MFUMO WA KUONDOA 'JANJAJANJA' KATIKA UNUNUZI WA UMMA WAJA

MAMLAKA ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), imetangaza kuwa kuanzia Julai Mosi mwaka huu, itatumika mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi (NeST) ili kuondoa kero zilizojitokeza katika sekta hiyo...

UKURASA WA 9

## TAKUKURU KUCHUNGUZA TUHUMA UPOTEVU MIFUKO SARUJI UJENZI WA ZAHANATI

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru, Abdala Shaib Kaim, ametoa siku nne kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, kufanya uchunguzi wa madai ya upotevu...

VITA RUSSIA

## Wagner yasitisha uasi kuepusha umwagaji damu

UKURASA 19

**MICHEZO** KIKWETE AIFUNDA TFF KWA MAYELE, BALEKE UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Kero za wananchi zilivyoishtua CCM

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema amechoshwa na kero ya migogoro ya ardhi katika Mkoa wa Dodoma, akiagiza mamlaka zinazohusika kuitatua haraka.

Chongolo alitoa kauli hiyo jana alipohutubia mkutano wa hadhara uliofanyika Uwanja wa Mtekelezo jijini Dodoma wakati wa kuhitimisha ziara yake mkoani hapo.

Alisema amechoshwa na tatizo la migogoro ya ardhi hasa katika Jiji la Dodoma ambalo lina malalamiko mengi ya wananchi kuhusu ardhi.

"Zamani Halmashauri ya Kinondoni iliongoza kwa migogoro ya ardhi Tanzania lakini kwa sasa mkoa unaoongoza kwa migogoro na kitovu cha migogoro ya ardhi nchini ni Dodoma na sababu ni tabia zetu wenyewe.

"Hakuna mgogoro wa ardhi uliotoka mbinguni ukashuka na kuwakuta watu wakiwa salama na kuwa mgogoro, mgogoro wowote unaoitwa mgogoro wa ardhi yupo mtu anautengeneza, hatuwezi kukaa kila siku tunazungumza migogoro," alionya.

Alisema Dodoma ni makao makuu ya nchi, hivyo hawawezi kupaacha pakawa kitovu cha migogoro. Wanataka pawe sehemu ya maendeleo kwa sababu ni sura ya nchi.

Alisema CCM wataingilia migogoro hiyo ili kuondoa malalamiko ya wananchi kuhusu ardhi, hivyo wahusika wachukue hatua ya kutatua migogoro hiyo.

Chongolo aliiagiza Wizara ya Ardhi pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutatua migogoro hiyo katika mkoa huo na maeneo mengine nchini.

Mbunge wa Dodoma, Anthony Mavunde, akitoa salamu za jimbo hilo, alilalamikia suala la mgogoro wa ardhi kuwa ni tatizo kubwa jimboni.

**NDUGAI NA BANDARI**

Spika mstaafu, Job Ndugai, akizungumza kwa niaba ya wabunge wa Mkoa wa Dodoma, alisema anaunga mkono uamuzi wa serikali wa kuita wawekezaji wa nje katika bandari za Tanzania.

"Dunia inabadilika na baada ya dunia kubadilika mambo yamebadilika. Mwingereza alikuwa akijivunia kampuni ya Landrover, leo mwenye hisa nyingi ni Mhindi, hata Waingereza wao hawaelewi katika hili, ndiyo utandawazi," alisema.

Alitaja kero nyingine mkoani Dodoma mbali na migogoro ya ardhi, ni uhaba wa maji katika maeneo mbalimbali na utatuzi wake unafanyika kwa kusuasua.



Naibu Kadhi Mkuu wa Tanzania, Sheikh Ally bin Muhidin Mkoyokole, akifungua jiwe la uzinduzi rasmi wa Msikiti wa Taqwa Mtakanini uliojengwa na mkazi wa kijiji hicho, Ramia Yasin, jana. Kushoto ni Rais mstaafu, Jakaya Kikwete na Mbunge wa Namtumbo, Vita Kawawa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia aagiza waraibu dawa za kulevya wapewe mikopo ya 10%

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameiagiza Ofisi ya Waziri Mkuu wakati inaandaa miongozo na utaratibu mpya wa kutoa mikopo ya asilimia 10, waraibu wa dawa za kulevya wajumuishwe, ili washiriki katika ujasiriamali utakaowainua kiuchumi.

Vilevile, ameagiza watendaji wa ofisi yake - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Afya na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kuweka mikakati ya pamoja ya kutoa afua kwa waraibu ambao afya zao zinaimarika ili wasirudie kutumia dawa za kulevya.

Jijini Arusha jana katika kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya kupiga vita dawa za kulevya duniani, Rais Samia alisema athari za dawa za kulevya, hasa kwa vijana, ni kubwa na kuwataka kujiepusha kuiga kila kitu.

"Katika ripoti ya kamati iliyoundwa na Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa ya dawa za kulevya, nimebaini jitihada kubwa zinatakiwa zielekezwe kutibu kwa kuwaunganisha waraibu na kliniki," alisema.

Rais alisema vijana wanaomaliza tiba wanarejea katika matumizi ya dawa za kulevya kwa kuwa hawana kazi ya kufanya.

"Waziri Mkuu umewasikia waraibu wanasema wanapoacha matumizi ya dawa hizi, wanakosa cha kufanya na baadhi hurudi katika matumizi ya dawa hizi. Sasa ninakuangiza mnapoandaa mfumo na utaratibu wa kutoa mikopo ya asilimia 10 ambayo tulisitisha na waraibu wawekwe katika mpango huo.

"Vilevile, wizara hizi tatu nendeni mkakae kwa pamoja mweke utaratibu mzuri wa namna ya kutoa afua kwa waraibu hawa, ili wasirejee tena katika matumizi ya dawa hizi ambazo zinaathiri nguvu kazi ya Taifa," aliagiza.

**MBINU MPYA**

Rais Samia pia aliziagiza mamlaka zote za serikali kufuatilia mbinu mpya za wafanyabiashara wa dawa za kulevya, ikiwamo kuchanganya na moshi unaotolewa katika 'Exsoze' za magari na mafundi gereji na kuuza kwa wafanyabiashara hao. Alisema jambo hilo ni hatari kwa kuwa kinachotolewa katika gari ni sumu.

"Unga wa moshi wa magari unachanganywa na dawa za kulevya na kuuzwa kwa vijana wetu na hii ni hatari kwa afya zao kwa sababu baadhi yao hupoteza hata maisha," alisema.

**KISIMIRI JUU**

Kuhusu maombi yalitotolewa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Kisimiri Juu, Mbayani Korisoi, kuhusu shughuli mbadala, Rais aliagiza Wizara ya Kilimo kufanya utafiti wa mazao yanayostawi katika kijiji hicho ili wananchi waanze kulima mazao mbadala wa bangi.

Eneo hilo linaongoza kwa kilimo cha bangi na mwanzoni mwa mwezi huu ekari 100 ziliteketezwa, huku ikielezwa bangi ya eneo hilo ni kali.

"Nimesikia changamoto yenu ya maji ya matumizi ya nyumbani na kumwagilia mazao, pamoja na miundombinu mibovu ya barabara. Hayo ni majukumu ya serikali. Nitahakikisha ninatatua changamoto hizi, lakini niwaombe viongozi msiwe sehemu ya kilimo cha bangi, lindeni kilimo hicho kisiendelee," alisisitiza.

Alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa jamii hasa wazazi na walezi kujikita katika malezi ya vijana wao, ili kunusuru kizazi hicho.

"Tatizo hili ni kubwa nchini na hii haiangalii hadhi ya familia wala jinsia, hivyo ninawaomba wazazi na walezi tufuatilie mienendo ya watoto wetu, ikiwa ni pamoja na kujikita katika malezi kwa sababu watoto wengi wa mitaani wana wazazi na wengi wao ni watumiaji wa dawa za kulevya kutokana na kukosa malezi bora," alisema.

Rais Samia alipongeza Malamka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kazi kubwa inayoifanya kukabiliana na biashara ya dawa ya kulevya, akiahidi kuendelea kutatua changamoto zinazoikabili.

Alitoa angalizo kwa taasisi zote zinazohusika na mwenendo wa kesi mbalimbali zinazohusiana na dawa za kulevya kuzingatia weledi wakati wa kutekeleza majukumu yao ikiwa pamoja na kutowabambika watu kesi.

"Baadhi ya kesi zinazokwenda mahakamani zinazohusiana na dawa za kulevya serikali inashindwa kutokana na kutowasilishwa vielelezo sahihi na ushahidi kuwa na upungufu.

"Hivi karibuni nitapokea taarifa ya hakijinai na mimi ninaamini italeta mabadiliko katika usimamizi wa hakijinai zikiwamo kesi za dawa za kulevya," alisema.

Awali Kamishna Jenerali wa DECA, Aretas Lyimo, alishukuru serikali kwa kutoa Sh. bilioni 2 kwa ajili ya ujenzi wa kituo kitakachotoa mafunzo ya ufundi stadi kwa waraibu jijini Dodoma.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha miezi mitatu, wamekamata kiwango kikubwa cha bangi na watuhumiwa 109.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema serikali imeweka nguvu kubwa katika Kijiji cha Kisimiri Juu, ambacho ni maarufu kwa kilimo cha bangi.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Korisoi, aliiomba serikali kuwajengea miundombinu ya barabara na maji ili waachane na kilimo cha bangi.

Baadhi ya mashuhuda wa dawa za kulevya, wakiwamo Judith Uloki na Twaha Mtunga, waliomba serikali kuwasaidia mitaji ili wafanye shughuli za ujasiriamali.

Judith alisema alifundishwa na mume wake matumizi ya dawa za kulevya na kumsababishia kupita katika kipindi kigumu, hata kupelekwa gerezani baada ya kulazimika kuiba ili apate fedha za kununua dawa za kulevya.

# ‘Kitabu cha IGP Mwema ni darasa kwa polisi’

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, amesema kitabu alichokiandika Mkuu wa Jeshi la Polisi mstaafu, Saidi Mwema, kitakuwa funzo kwa askari nchini katika kufikia jeshi lenye weledi na utii wa sheria.

Wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu hicho jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Sagini alisema kimebeba mambo mengi ya muhimu na hivyo jeshi hilo linapaswa kukitumia kujifunza na kuyafanyia kazi maudhui yaliyomo.

Alisema kitabu hicho chenye sura tisa kilichopewa jina la ‘Polisi Utawala na Usimamizi wa Sheria Tanzania Mkakati Kubadilisha Mwelekeo’, kinaweza kubadili utendaji kazi wa Jeshi la Polisi katika nyanja mbalimbali ikiwamo usimamizi wa sheria, haki na jukumu la msingi la kuanzishwa kwa jeshi hilo - usalama wa raia na mali zao.

Sagini aligusia maudhui ya kitabu hicho kwamba kinaliasa Jeshi la Polisi kuendana na teknolojia, mwandishi wake akisisitiza wezi wamekuwa wakibadilika na sasa wanaiba kidigitali zaidi, hasa wizi kupitia mitandaoni.

“Kilichomo katika kitabu hicho, pia kinaonyesha jinsi historia ya mapito na maisha yake kiujumla. Pia kinagusia ushirikiano mzuri alioupata kwa Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, ambaye amemtaja kuwa alikuwa ni mtu mkarimu na alipenda kumtia moyo wakati wote.

“Kwa hiyo, kitabu hiki Wizara ya Mambo ya Ndani tutahakikisha tunakigawa kwa Jeshi la Polisi na mamalaka zake zote, ili waweze kukisoma na kuutumia utaalamu huo kutimiza majukumu yao ya kila siku,” aliahidi.

Katika hafla hiyo, Mwandishi wa Kitabu hicho, Mwema, alikitaja ni zawadi kwa Watanzania na Jeshi la Polisi ili ‘kuwaambukiza’ ujuzi wake.

Alisema kitabu hicho pia kimebeba historia ya nchi na namna jeshi hilo lilivyoyumba na kuimarika. Alikitaja ni andiko la urithi, hazina, ujuzi, uzoefu na mbinu.

“...kimesheheni mambo mengi mazuri, elimu na mafunzo kuhusu jeshi letu, kazi na wajibu wa maofisa na askari wetu. Pia kinatoa mwelekeo thabiti katika kutatua vikwazo vinavyolikabili jeshi katika karne hii ya 21.

“Kimeangalia athari za utandawazi katika usimamizi wa sheria na kusisitiza umuhimu wa kuwa na mtazamo mpya na mikakati katika kuhakikisha usalama unaendana na mabadiliko ya kiuhalifu,” alisema Mwema na kusisitiza hakiuuzwi. Kimechapwa kwa ulifadhili na Shirika lisilo la kiserikali la Hanns Seidel Foundation (HRS).




Hafla ya uzinduzi wa kitabu hicho ilihudhuriwa na viongozi na maofisa mbalimbali wakiwamo: Jaji Mkuu mstaafu na Mwenyekiti wa Tume ya Hakijinai, Othman Chande, Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Balozi Ombeni Sefue, Mkuu wa Jeshi la Polisi mstaafu, Ernest Mangu na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Hanns Seidel Foundation, Karl-Peter Schöndorfich.

## Benki yajitosa kukabili magonjwa ya mlipuko

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya Biashara nchini (TCB) imesema itahakikisha inashirikiana na wafanyabiashara katika nyanja mbalimbali kuimarisha usafi wa mazingira mahala pa kazi ili kuondokana na magonjwa ya mlipuko.

Meneja wa TCB, Tawi la Kigamboni, Lameck Buberwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi kwa Umma.

Benki hiyo iliadhimisha siku hiyo kwa kukabidhi vifaa vya usafi katika Soko la Samaki Ferry, Kivukoni jijini kwa kutambua umuhimu wa huduma wanayoitoa.

Alisema soko hilo ambalo limekuwa linatoa huduma ya chakula, linapaswa kuwa safi muda wote kutokana na kuwapo msongamano mkubwa wa watu ili mlipuko wa magonjwa usitokee.

“Tunaomba mpokee vifaa hivi. Huu ni mwanzo, tutaendelea kushirikiana zaidi hata katika kukamilisha miradi kupitia huduma zetu za kibenki tunazozitoa ikiwamo kufungua akaunti na utoaji mikopo ya riba nafuu,” alisisitiza.

Meneja huyo aliendelea kusisitiza ushirikiano wa viongozi wa soko hilo ili kuinua vipato vyao ikiwamo kuwafungulia akaunti na kuwapa elimu ya matumizi ya fedha ili wakikopa wasifilisike kwa kushindwa kurejesha mikopo.

Ofisa Afya wa soko hilo, Mary Mkwavi, aliishukuru benki hiyo kwa kuwapatia vifaa hivyo, akisema usafi haukwepeki.

“Vifaa hivi vitawasaidia kusafisha soko na kuwa na mandhari nzuri zaidi, isiishie hapa, watukumbuke mara kwa mara,” alisisitiza.

Kaimu Mkuu wa soko hilo, Ally Kasembe, alisema kuna umuhimu taasisi za kifedha kuwa karibu na wafanyabiashara wa soko hilo na kuwashawishi kufungua akaunti, kukopa na kuhifadhi fedha zao benki.

## Oryx yakamilisha ujenzi bomba la kusafirisha gesi

**Na Restuta James**

KAMPUNI ya Oryx Gas Tanzania imekamilisha ujenzi wa bomba kubwa la kusafirisha gesi kutoka kwenye meli bandarini kwenda kwenye bohari yake iliyoko Kigamboni, Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza muda wa kupokea gesi.

Jijini Dar es Salaam jana, Meneja Masoko wa Oryx Gas Tanzania, Peter Ndomba, alisema kukamilika kwa ujenzi wa bomba hilo lenye ukubwa wa nchi 10, kutarahisisha utoaji huduma kwa wateja wakubwa wa gesi ya Oryx.

Alisema nia ya kuboresha miundombinu ya Oryx, ni kuunga mkono ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, kutoka asilimia tano ya sasa hadi asilimia 80.

Ndomba alisema mbali ya kuongeza ukubwa wa bomba kutoka nchi sita hadi 10, kampuni hiyo inakusudia kuongeza ukubwa wa tangi la kuhifadhia gesi.

“Zaidi ya hapo tumekuwa tukigawa mitungi kwenye taasisi na makundi mbalimbali ya wananchi,” alisema. Alifafanua kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja, kampuni hiyo imegawa mitungi ya gesi na majiko zaidi 7,000, kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Awali, Meneja Miradi wa Oryx Gas Tanzania, Joseph Soka alisema ujenzi wa bomba la kupokelea gesi kutoka KOJ kwenda bohari ya Oryx Gas iliyoko Kigamboni ulikamilika Juni 17, mwaka huu.

“Tulipokuwa tunatumia bomba dogo tulikuwa tunapokea mzigo kutoka katika meli kwa muda usiopungua saa 30 kwa mzigo wa metriki tani 2,500. Baada ya kuongeza ukubwa wa bomba la kupokelea gesi sasa tunaweza kupokea ujazo ule ule kwa muda saa 20,” alisema.

Soka alisema bomba hilo lenye urefu wa kilometa 2.8. Kati yake, mita 960 zinapita baharini. Lilianza kujengwa Desemba 5, 2022.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

eGA

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU**

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara wa vifaa chakavu yakiwemo magari, samani za ofisi pamoja na vifaa vingine siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dar es Salaam na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku ya Jumapili tarehe 25 Juni, 2023 katika Jengo la UTUMISHI Kivukoni Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo ambavyo ni viti vya ofisini “Office Chairs”, “Printers” na “Laptops” na siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni katika Ofisi za e-GA Mji wa Serikali Mtumba Dodoma kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa hivyo, ambapo pamoja na vifaa vingine, magari yote yameegeshwa katika ofisi za e-GA.

**Maelezo zaidi ya magari hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali:**

| Na | Aina | Modeli | Namba ya Usajili | Mahali lilipo | Hali ya Gari |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA station wagon Diesel Engine | LAND CRUISER V8 | STL2039 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 2 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine, | PAJERO ST WAGON | STL2011 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |
| 3 | Mitsubishi Pajero 4WD, Station Wagon with 2.8L Diesel Engine | PAJERO ST WAGON | STL2010 | e-GA HQ Mtumba Dodoma | Halitembei |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari hayajalipiwa ushuru na kodi ya ongezeko la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru na kodi zingine kabla ya kulichukua toka Mamlaka ya Serikali Mtandao
2. Magari yatauzwa kama yalivyo mahali yalipo
3. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana “deposit” isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa kwa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichopata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi (on fall of the hammer). Kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia mnunuzi atakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo mara tu baada ya kulipia (cash and carry)
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 27 Juni katika ofisi zake za Dar es Salaam, 2023 na Alhamisi tarehe 29 Juni, 2023 katika ofisi zake za Dodoma.

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mkuu**

**Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz
“Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma”

# Mwanasheria achambua kifungu kwa kifungu mkataba wa Bandari

Na Restuta James



MWANASHERIA Mwandamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Kulwa Mumbuli, amechambua vifungu vinavyoonekana kuwa na 'utata' katika makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi na kijamii (IGA) kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai.

Pia amesema mchakato wa kuandaa IGA ni mrefu, ukihusisha wataalamu mbalimbali wenye weledi kwa nia ya kuhakikisha maslahi ya nchi yanazingatiwa.

Mumbuli alichambua makubaliano hayo ya IGA ambao Nipashe imeona nakala yake, alipozungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Akianza na Ibara pili ya IGA inayozungumzia malengo ya mkataba, Mumbuli alisema kifungu hicho kimetafsiriwa vibaya na baadhi ya watu aliowaita "wapotoshaji", wanaodai kampuni ya DP World itakabidhiwa bandari zote za bahari na maziwa huku wakijua kwamba kiambatanisho namba moja kimetangaza magati 0, 1-4 na 5-7 ya Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema ibara ya tatu ya IGA ambayo inaeleza kuhusu ushirikiano, kifungu cha (2)(a) kinaeleza kuwa nchi washirika zitaunda kamati moja ya ushauri ambayo pamoja na mambo mengine, itafanya ukaguzi na kubadilishana taarifa mara kwa mara kwa mamlaka zinazohusika.

"Kiambatisho Na. 1 kinaeleza kwamba DPW ataendeleza, kusimamia na kuendesha "RoRo Terminal (Berth 0), Genaral Cargo Terminal (Berth 1-4) na Container Terminal (Berth 5-7) za Bandari ya Dar es Salaam.

"Kwa hiyo majadiliano ya HGA na mikataba ya utekelezaji yatajikita katika maeneo hayo. Kwa hiyo, hakuna sehemu yoyote kwenye mkataba wa IGA inayosema DP World atachukua bandari zote za Tanzania," alisema Mumbuli.

Aliongeza kuwa ibara ya 5 inayozungumzia haki ya kuendeleza, kusimamia au kuendesha, imeyalenga magati yaliyoainishwa katika kiambatanisho cha kwanza ambayo ni gati 0, 1-4 na 5-7.

Alisema anaowaita "wapotoshaji" wamekitumia kifungu hicho kuzungumzia haki za mwekezaji, bila kueleza kuwa hana haki katika bandari zingine wala magati namba 8-11, yaliyosalia katika Bandari ya Dar es Salaam.

**MIAKA 100**

Kuhusu IGA kuweka kipengele cha miaka 100 na sharti la kutorekebisha mkataba wala kuvunja, Wakili Mumbuli, alisema hakuna sehemu pande hizo mbili zimekubaliana miaka wala masharti hayo.

Alisema ibara ya 22 ya makubaliano hayo inazungumzia mapitio na marekebisho ya IGA. "Pamoja na mambo mengine, ibara hii inaeleza kuwa makubaliano haya yanaweza kurekebishwa wakati wowote, kwa maandishi na mazungumzo ya pande zote za serikali," alisema.

Aliongeza kuwa ibara ya 23 inaeleza muda wa mkataba na namna ya kuvunja na kwamba serikali za pande zote zimepewa idhini ya kusitisha makubaliano hayo, kwa kuutaarifu upande mwingine.

"Ukienda Ibara ya 20, utaona kwamba kuna utaratibu wa kutatua mgogoro... wanaosema mkataba hauvunjiki wanalenga nini wakati kuna kipengele kinachoweka utaratibu wa kutatua migogoro?" alihoji.

Kwa mujibu wa ibara hiyo ambayo iko ukurasa wa 26 na 27 wa IGA, pande hizo zimekubaliana kutatua migogoro kwa njia mbili.

**MGOGORO UKITOKEA**

Kifungu cha kwanza cha ibara hiyo kinaeleza kuwa pindi mgogoro ukitokea baina ya pande hizo, njia ya kwanza itakayotumika ni ya mazungumzo.

"Mzozo unaotokana na, au unaohusiana na makubaliano haya utawasilishwa na (upande husika), kwa utatuzi kwa njia ya kidiplomasia au, ikiwa sehemu hiyo itachagua, kamati ya mashauriano ya IGA," inaelezwa katika kifungu hicho.

Inafafanuliwa zaidi kuwa ikiwa mzozo haujatatuliwa kwa amani ndani ya siku 90, upande usioridhika utautaarifu mwingine kuwa mgogoro haujaisha.

Kifungu cha pili cha ibara hiyo kinazungumzia namna usuluhishi utakavyofanyika na kwamba upande usioridhika utampa mwenzake notisi ya siku 30 ya kueleza nia yake ya kwenda Baraza la Usuluhishi, litakalowasuluhisha kwa kutumia Sheria za Umoja wa Mataifa (UNCITRAL).

Kifungu hicho kinaeleza kuwa usuluhushi utafanyika jijini Johannesburg, Afrika Kusini.

"Kwa kuwa IGA inalinda uhusiano wa taifa na taifa, migogoro inayotokana na vipengele vya IGA haiwezi kutatuliwa na mahakama za taifa mojawapo kati ya mataifa hayo mawili yenye mgogoro; ambayo ni pande za mkataba wa IGA.

"Kwa hiyo mgogoro wa aina hii daima hutatuliwa na vyombo vya kisheria vya taifa lingine lisilofungamana na upande wowote wa mkataba husika (IGA). Hii ndiyo sababu ya migogoro itakayotokana na IGA kwenda kutatuliwa Afrika Kusini," alifafanua.

Ibara ya 21 inaeleza kuwa sheria zitakazosimamia IGA ni za Uingereza wakati zitakazosimamia mikataba ya utekelezaji kati ya DP World na TPA, ni za Tanzania.

Mumbuli alisema Ibara ya 27 imetafsiriwa vibaya na baadhi ya watu kwa kuwa jambo la busara kuingia makubaliano ya kuendesha gati 0, 1-4 na 5-7 na nchi nyingine ilhali Tanzania iko kwenye mazungumzo na Dubai.

"Ni kama vile umeshapata mtu ambaye ameonyesha nia ya kupanga nyumba yako na wakati huo huo unaita mtu mwingine kumpangisha hapohapo. Kibiashara hasa za kimataifa zinazohusisha kujenga uhusiano, hili halijengi taswira nzuri," alisema.

Aliongeza kuwa nia ya kifungu hicho ni kuihakikishia nchi husika kwamba Tanzania iko tayari kwa ushirikiano wa kiuchumi na kijamii na haina nia ovu, kutunga au kuingia katika ushirikiano utakaokwaza IGA kati yake na Dubai.

Kifungu kingine kinachodaiwa kupotoshwa kwa mujibu wa Mumbuli, ni cha 14 kinachozuia utaifishaji wa mali za DP World.

Wakili huyo alisema kifungu hicho kimewekwa ili kumhakikishia mwekezaji kwamba serikali ina nia thabiti ya kuendeleza rasilimali zake na pia kuheshimu mikataba ya kimataifa.

"Wapotoshaji wanasoma kifungu kwa nia mbaya bila kusoma ibara ya 21 inayosema mikataba ya utekelezaji itasimamiwa na sheria za Tanzania," alisema.

Aliongeza kuwa matukio yoyote ya kijinai na ukiukwaji wa sheria za nchi wakati wote wa mkataba kati ya TPA na DP World; ambayo yatafanywa na kampuni hiyo, yatahukumiwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

"Kusema hatutataifisha haina maana kwamba akihujumu uchumi tutakaa kimya. Akifanya udhalilishaji wa wafanyakazi tutanyamaza. Mwekezaji atatakiwa kuzingatia sheria zote za nchi; na hili liko ndani ya mkataba huu wa IGA," alisema.

Wakili Mumbuli alisema IGA imeweka sharti la mwekezaji kuheshimu sheria za nchi na akikiuka anashtakiwa na kuhukumiwa bila ubaguzi au upendeleo.

**HISA, BRELA**

Mwanasheria huyo pia alisema kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni, Kampuni ya DP World haiwezi kuanza shughuli zake nchini bila kujisajili kwa Wakala wa Usajili wa Biashara (BRELA) ambayo pia inataka mgeni asimiliki kampuni kwa asilimia 100 peke yake.

Alikumbusha kuwa sheria hiyo inamtaka amiliki asilimia zisizozidi 51 ya hisa na kutoa hisa nyingine kwa kampuni inayomilikiwa na Mtanzania.

Alisema sharti lingine ni kama kampuni hiyo itataka kuwekeza kwenye Ukanda Maalum wa Biashara (EPZA) au kupitia Kituo cha Uwekezaji (TIC), mwekezaji atalazimika kutimiza kiwango cha mtaji anachopaswa kuwa nacho.

Kuhusu uandaaji wa IGA hadi inatiwa saini, Mumbuli alisema sekta husika huandaa andiko linalopita katika mchakato wa wataalamu wa ngazi tofauti hadi kwenye kamati ya makatibu wakuu ambao huipeleka Baraza la Mawaziri.

"Katika ngazi zote, maoni na maboresho yanafanywa kuhakikisha tunalinda maslahi ya nchi. Tumeyazingatia kwa sababu na sisi ni Watanzania, tuna uchungu na nchi yetu pia," alisema.

Tangu kutolewa taarifa ya kuwapo hoja ya Bunge kupelekewa azimio la kuridhia ushirikiano, kumekuwa na mjadala mkali, ikiwamo katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu mpango huo wa serikali.

**TANGAZO**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz
NFRA


# TANGAZO KWA UMMA

## VITUO VYA UNUNUZI WA AKIBA YA CHAKULA YA TAIFA KWA MSIMU WA 2023/2024

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kuzungusha akiba ya chakula ili kukabiliana na upungufu wa chakula na majanga mengine ya Kitaifa yanayoweza kujitokeza. NFRA hununua nafaka kila mwaka kwa ajili ya akiba ya chakula ya Taifa. Kwa msimu huu wa mavuno ununuzi umeanza rasmi tarehe 22 Juni, 2023.

Wakala unategemea kutumia vituo kwenye mikoa mbalimbali, ambavyo vitakua vinafunguliwa kwa kuangalia hali ya ukaukaji wa nafaka, uzalishaji wa ziada wa zao husika (mahindi na mpunga), eneo kuwa na ghala zuri la kuhifadhia nafaka, bei ya soko, usalama wa eneo, mgawanyiko wa kijiografia na kuwepo na huduma muhimu.

Kwa kuanzia, NFRA itafungua vituo vya ununuzi wa mahindi kwenye kanda zifuatazo zenye uzalishaji na upatikanaji mkubwa wa nafaka; Songea (Mkoa ya Ruvuma), Makambako (Mikoa wa Njombe na Iringa), Songwe (Mikoa wa Songwe na Mbeya), Sumbawanga (Mikoa ya Rukwa na Katavi), Dodoma (Dodoma na Manyoni), Arusha (Arusha na Manyara) na Shinyanga (Mkoa wa Kigoma na Tabora). Aidha, mpunga utanunuliwa katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Songwe, Mbeya na Tabora.

**MCHANGANUO WA VITUO VYA UNUNUZI WA NAFAKA NA BEI KWA MSIMU WA 2023/2024**

| Na. | KANDA | MKOA | WILAYA | KITUO | BEI (TZS) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | MAHINDI | MPUNGA |
| 1 | ARUSHA | Arusha | Karatu | Karatu | 900-1,000 | |
| | | Manyara | Babati | Babati | | |
| 2 | DODOMA | Dodoma | Dodoma Mjini | Kizota (Ghala kuu) | 700-800 | |
| | | Manyara | Kiteto | Kiteto | | |
| 3 | KIPAWA | Morogoro | Mvomero | Mvomero | | |
| | | Tanga | Handeni | Handeni | 800 | |
| 4 | MAKAMBAKO | Iringa | Kilolo | Ilula | 700-800 | 900-1,000 |
| | | | Iringa Vijijini | Pawaga | | |
| | | Njombe | Ludewa | Mlangali | | |
| | | | | Shaurimoyo | | |
| | | | Njombe DC | Makambako (Ghala Kuu) | | |
| | | | Wanging'ombe | Igula | | |
| | | Mbeya | Mbalali | Uturo | | |
| | | | | Madibira | | |
| | | | | Chimala | | |
| 5 | SHINYANGA | Shinyanga | Shinyanga Mjini | Shinyanga (Ghala kuu) | 750-950 | 900-1,000 |
| | | Tabora | Nzega | Bukene | | |
| | | Kigoma | Kasulu | Mvugwe | | |
| 6 | SONGEA | Ruvuma | Songea Mjini | Ruhuwiko (Ghala Kuu) | 650-700 | |
| | | | Songea Vijijini | Magagura | | |
| | | | | Mgazini | | |
| | | | Madaba Mji | Madaba | | |
| | | | Mbinga | Mbinga | | |
| | | | Namtumbo | Namtumbo | | |
| | | | Nyasa | Tingi | | |
| | | | Tunduru | Tunduru | | |
| 7 | SONGWE | Songwe | Mbozi | Vwawa (Ghala Kuu) | 650-800 | 900-1,000 |
| | | | Ileje | Isongole | | |
| | | | Momba | Kakozi | | |
| | | | Momba | Nkala | | |
| | | | Momba | Chitete | | |
| | | | Momba | Naming'ong'o | | |
| | | Mbeya | Mbeya Vijijini | Inyala | 700-800 | 900-1,000 |
| | | | Kyela | Makwale | | |
| | | | Kyela | Ngana | | |
| 8 | SUMBAWANGA | Rukwa | Sumbawanga mjini | Mazwi (Ghala Kuu) | 600-800 | |
| | | | Sumbawanga vijijini | Laela | | |
| | | | | Mtowisa | | |
| | | | Kalambo | Mwimbi | | |
| | | | Nkasi | Namanyere | | |
| | | Katavi | Mpimbwe | Majimoto | 600-800 | |
| | | | Mlele | Kibaoni | | |
| | | | Tanganyika | Sibwesa | | |
| | | | | Kasekese | | |

**Utaratibu wa Ununuzi:**
Nafaka zote zitakazofikishwa katika vituo vya NFRA, zitapokelewa iwapo zitakidhi vigezo vya ubora kama vitakavyobainishwa kupitia Kanda za NFRA. Bei elekezi zitakazotumika zitapangwa kwa kuzingatia umbali kutoka ghala kuu la NFRA na bei za soko katika eneo husika. Utaratibu wa ununuzi wa nafaka kupitia Vyama vya Ushirika/Vikundi vya Wakulima, Wafanyabiashara na Mawakala utafanyika kupitia makubaliano yatakayofikiwa baina ya makundi hayo na Kanda za NFRA.

**Utaratibu wa Malipo:**
Malipo yote yatafanyika ndani ya siku tatu baada ya kukamilisha taratibu za kupokea nafaka.

Kwa maelezo zaidi kuhusu vituo vya ununuzi, utaratibu wa ununuzi na bei katika vituo husika, wasiliana na Meneja wa Kanda/Vituo vya NFRA vilivyo karibu yako.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA)**
**20 Juni, 2023.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wawakilishi wa nchi michuano Caf fanyeni usajili makini sasa

**KUELEKEA** msimu mpya wa 2023/24 wa michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika, kwa mara nyingine tena Tanzania itawakilishwa na timu nne, Simba, Yanga, Azam FC na Singida Fountain Gates FC.

Timu mbili, Simba na Yanga zitabeba jukumu hilo kwenye Ligi ya Mabingwa wakati Azam FC na Singida Fountain Gate FC, zikiwa na fursa hiyo katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hii ni michuano ambayo wawakilishi wanapaswa kujipanga vema ndani na nje ya uwanja kuanzia usajili, mabenchi ya ufundi na zaidi kuhakikisha zinakuwa imara kiuchumi.

Tunasema wawakilishi hao wanapaswa kujiandaa zaidi pia kiuchumi hasa tukikumbuka aibu iliyotokea msimu wa 2021/2022 kwa timu ya Biashara United kushindwa kwenda Libya kucheza mechi yao ya marudiano dhidi ya Al Ahly Tripoli, hivyo kutolewa wakati tayari ilikuwa na uongozi wa mabao 2-0 katika mchezo wa mkondo wa kwanza nyumbani.

Hivyo, hatutarajii kuona tena aibu hiyo ikitokea kwani tunaamini timu zilizofuzu kuiwakilisha nchi zinatambua ni gharama kiasi gani inawakabili katika ushiriki wao, lakini pia zimejipanga kiuchumi.

Mbali na hilo, katika suala zima la ndani ya uwanja eneo ambalo ndilo kiu kubwa la mashabiki na Watanzania kwa ujumla kutaka kushuhudia soka la kuvutia na timu zao zikipata ushindi na kufika fainali kama si kulibeba kabisa taji, hapa panahitaji jicho la ziada mapema katika kipindi hiki cha usajili.

Ingawa Shirikisho la Soka nchini (TFF), kupitia kwa Bodi yake ya Ligi (TPLB), bado hawajatangaza tarehe rasmi ya kufunguliwa kwa dirisha la usajili kuelekea msimu mpya, lakini huu ni muda ambao wawakilishi wetu hao wanapaswa kumaliza biashara hiyo mapema.

Tunatambua muda ni mchache sana, na hata dirisha la usajili litakapofunguliwa linaweza kuwa wazi kwa kipindi cha mwezi mmoja tu, muda ambao ili kuweza kwenda na wakati, zinabidi kumaliza biashara hiyo mapema ili dirisha litakapofunguliwa ziwe zinakamilisha tu kuwasajili katika mfumo rasmi wa TFF.

Tayari baadhi ya klabu zimekamilisha mazungumzo na kutoa mikataba ya awali kwa wachezaji zinaowataka kuwasajili, jambo ambalo ndilo tunatamani kuona likifanywa na klabu zote zenye jukumu la kuiwakilisha nchi kimataifa.

Matarajio yetu ni kuona pindi dirisha la usajili litakapofunguliwa wawakilishi hao wawe wanakwenda kuwahalalisha nyota wao wapya katika mifumo ya TFF na kisiwe kipindi cha kuanza mazungumzo na wachezaji wanaowataka, jambo ambalo pia litazisaidia klabu husika kwenda kujiandaa na msimu mpya zikiwa tayari na vikosi vyao kamili.

Lakini kuna faida kubwa ya kumaliza biashara mapema kwani baadaye gharama za kununua wachezaji pindi ligi zote barani Afrika zinapomalizika, huwa kubwa mno na ni vigumu kwa klabu zetu kuweza kushindana sokoni na klabu kubwa Afrika na Ulaya.

Aidha, hatutarajii kuona tena baadhi ya wawakilishi wetu hao kimataifa panatokea klabu inaelekea kujiandaa na msimu mpya (pre-season), huku ikiwa haijakamilisha idadi ya wachezaji inaotaka kuwasajili, kwani kwa kufanya hivyo kutamtibulia kocha kuweza kutekeleza programu zake vizuri.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mashujaa imestahili kupanda Ligi Kuu

**KATIKA** mechi zote za 'play off' zilizochezwa msimu huu, kuanzia za Ligi Kuu mpaka Championship, iliyosisimuwa na kufuatiliwa na mashabiki wengi wa soka nchini ilikuwa ni kati ya Mashujaa FC ya Kigoma na Mbeya City.

Unaweza kusema mechi bora kabisa ya mchujo kuwahi kutokea tangu mfumo wa mechi hizo uanzishwe na Shirikisho la Mpira wa Miguu, TFF.

Achilia mbali mashabiki kujazana uwanjani, lakini kwenye vibanda umiza ndiyo zaidi. Mashabiki waliokuwa wanaiangalia mechi hiyo kwenye televisheni walianza kuvutiwa kuanzia ile ya kwanza iliyochezwa Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, ambako umati wa mashabiki uliojaa uwanjani ulishangaza wengi, hivyo kuwavuta watazamaji mchezo wa marudiano.

Mbali na hilo, aina yake ya ushangiliaji ilikuwa burudani tosha kiasi cha kuwa burudani kwa waliokuwa wakitazama na wala haikushangaza kwa muda mfupi tu, Mashujaa FC ikajipatia mashabiki wengi vibanda umiza.

Iliposhinda mabao 3-1 nyumbani, mashabiki wengi waliokuwa wakiangalia kwenye TV walionekana kuwa na furaha, lakini ilizidi zaidi juzi iliposhinda bao 1-0 kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya na kutinga Ligi Kuu.

Mechi ya marudiano ilijaza watu wengi si uwanjani tu, hata mitaani kwa waliokuwa wanaangalia kwenye TV baada ya kuridhishwa na burudani walioipata mechi ya kwanza ya mchujo.

Binafsi, naweza kusema mechi zote mbili za Mashujaa FC dhidi ya Mbeya City, ilizidi mechi nyingi za Ligi Kuu kwa kila kitu, kuanzia kujaza mashabiki, mvuto, mbwembwe za ushangiliaji na hata ubora tu wa mchezo uwanjani. Wachezaji walipambana na kujitoa kwa nguvu zao hasa wa Mashujaa na kuonekana kuwa wanaitaka hasa Ligi Kuu.

Waswahili wanasema Mungu humpa yule anayepambana, na kweli ilionekana kama isingekuwa haki kama Mashujaa FC wasingepanda Ligi Kuu. Kwa mtu aliyetazama mechi zote mbili anakubaliana nami.

Idadi ya jumla ya mabao iliyoshinda Mashujaa FC 4-2 kwenye mechi zote mbili inadhihirisha kuwa walidhamiria na waliitaka mno Ligi Kuu kuliko kitu kingine chochote.

Bahati mbaya kwa Mbeya City ilionekana kukumbuka shuka kumekucha. Awali ilidhania mechi yake ya 'play off' ingekuwa kama ile dhidi ya KMC au chini ya hapo. Mechi ile iliyochezwa na KMC ilikuwa ya kawaida sana, haikuwa na mvuto na kwa sababu iliona inakwenda kucheza dhidi ya Mashujaa iliyotoka Championship, wakaichulia poa.

Walichokutana nacho watasimulia siku zote. Walikutana na mechi ngumu nadhani kuliko wanazokutana nazo kwenye Ligi Kuu. Na 'nyomi' la mashabiki wa Kigoma likawashtua kuwa hawachezi na timu ya kawaida.

Ndiyo maana maandalizi ya mechi ya marudiano yakawa makubwa zaidi, lakini walikuwa wamechelewa.

Nadhani hili huwa linajirudia, huwa linashangaza na kukera. Mbeya City hadi inafika 'play off' ya pili, tena mechi ya marudiano, ndiyo hamasa zinaanza ikiwa pamoja kuruhusu mashabiki kuingia bure na kila aina ya msaada inatolewa ili kubaki Ligi Kuu.

Sidhani kama timu kama Mbeya City ilitakiwa kufika huko, kwani ilikuwa na uwezo hata wa kubaki Ligi Kuu hata 'play off' dhidi ya KMC. Wanasiasa na viongozi wao walisubiri hadi maji yamezidi unga.

Na nina hakika, lile nyomi la Kigoma, hamasa kwa wanasiasa wa huko, viongozi na aina ya soka lililochezwa na Mashujaa liliwatisha viongozi wa Mbeya nao wakaonekana kuwaiga wenzao. Vinginevyo nadhani isingekuwa vile tulivyoona.

Kilichotokea ni kwamba waliojipanga tangu mwanzo ndiyo waliofanikiwa. Narudia tena kusema Mashujaa FC walistahili kupanda na soka limetenda haki. Karibuni Ligi Kuu.

## TANGAZO

The Guardian
www.ippmedia.com

The Home of Great Newspaper

# Our Regional Offices and Representatives




*Feel free to contact for:*

**ADVERTISEMENT ON NEWSPAPERS / DIGITAL PLATFORMS AND SUBSCRIBING NEWSPAPERS / E-PAPERS**

**HEAD OFFICE**

THE GUARDIAN LIMITED
MIKOCHENI AREA
P.o.Box 31042, Dar es salaam, Tanzania
Tel: + 255 745700710 | Email: info@guardian.co.tz

Nipashe — @Nipashetz

The Guardian — @Theguardiantz

IPPmedia .com

# Wafanyabiashara wapewa elimu kulipa kodi kwa wakati

**Na Mwandishi Wetu,** BAHI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetoa elimu ya kodi kwa wafanyabiashara wilayani Bahi mkoani Dodoma, ikiwataka kulipa kodi kwa wakati ili kuepuka adhabu.

Akizungumza na wafanyabiashara wa wilaya hiyo wakati wa semina ya kutoa elimu hiyo mwishoni mwa wiki, Ofisa Msimamizi wa Kodi wa TRA, Joel Frael, aliwasisitiza wafanyabiashara kulipa kodi ya mapato awamu ya pili mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni mwaka huu ili kuepuka adhabu ya kutokulipa kodi kwa wakati.

Semina hiyo ilifanyika katika ukumbi wa mikutano Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Bahi, ikihudhuriwa na wafanyabiashara na viongozi wa wilaya hiyo.

Katika semina hiyo, wafanyabiashara walikumbushwa kutoa risiti sahihi za kielektroniki (EFD) wanapouza bidhaa kwa wateja na kudai risiti wanaponunua kuuza bidhaa kutoka kwa wafanyabiashara wenzao.

Ofisa Msimamizi wa Kodi, Philipo Eliamini, aliwapongeza wafanyabiashara kwa ushiriki wao katika semina hiyo.

Pia aliwakaribisha wafanyabiashara wa Bahi kufika katika ofisi za TRA zilizofunguliwa wilayani hapa.

"Nipende kuwakaribisha wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kufika katika ofisi zetu zilizopo hapa Bahi kwa huduma mbalimbali za kikodi.

"TRA imezidi kusogeza huduma kwa wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kwa kuhakikisha inafungua vituo vya huduma karibu na wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla," alisema.

Wafanyabiashara walioshiriki katika semina hiyo, waliipongeza TRA kwa kupeleka elimu ya kodi na kuahidi ulipaji kodi wa hiari kwa kuwa wengine wanashindwa kulipa kodi au kuchelewa kulipa kodi kwa kutokuwa na elimu sahihi ya kodi.

Pia waliomba TRA kuhakikisha inatoa elimu ya kodi kwa kila mfanyabiashara anayeonekana kukua na kuhamia katika aina nyingine ya ulipaji kodi ili kumjengea uelewa kuhusu masuala ya kodi.

Mfanyabiashara Emmanuel Kafulya alisema: "Elimu ya aina za kodi hususan VAT (Kodi ya Ongezeko la Thamani) inabidi itolewe kwa wale wote ambao wanakwenda kuingia katika mfumo kabla ya kuingizwa katika huo mfumo ili mfanyabiashara aelewe vizuri kabla ya kuingia katika huo mfumo wa ulipaji kodi."

TRA imekuwa inatoa elimu ya kodi kwa njia mbalimbali na juzi, elimu hiyo ilitolewa kwa njia ya semina maalum kwa wafanyabiashara wa wilaya hiyo.

# Mfumo wa kuondoa 'janjajanja' katika ununuzi wa umma waja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), imetangaza kuwa kuanzia Julai Mosi mwaka huu, itatumika mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi (NeST) ili kuondoa kero zilizojitokeza katika sekta hiyo.

Miongoni mwa faida za mfumo huo ni kuondoa wazabuni wasio na vigezo kuomba kazi wasizokuwa na utaalamu nazo na kupunguza mianya ya rushwa. Akitambulisha mfumo huo juzi jijini hapo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa PPRA, Dk. Leonada Mwagike, alisema Oktoba Mosi mwaka huu taasisi zote za umma zinapaswa kuanza kuutumia.

"PPRA imeanza kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo kwa kushirikiana na vyuo, moja ya nguzo kwenye mfumo ni kusajili watumiaji kwa haraka, urahisi na kwa usahihi, watumiaji wa mfumo wanatakiwa kujisajili na kuweka taarifa zinazotakiwa kwenye mfumo, unapatikana hadi kwenye simu za mkononi," alisema.

Alisema ili kuleta ufanisi, mfumo huo umeunganishwa na mifumo 14 ya serikali kurahisisha upatikanaji wa taarifa zinazohitajika kwa haraka na kwa usahihi.

"Moja ya mifumo iliyounganishwa ni BRELA, TAUS, TRA, GEPG, MUSE, CRB, ERB, OSHA, TIRA, TAMISEMI, Ofisi ya Msajili wa Hazina," alisema.

Alisema kuwa kutokana na mahitaji mapya ya teknolojia na maelekezo ya serikali ya kuimarisha eneo la ununuzi wa umma nchini hususan katika matumizi ya TEHAMA, PPRA ilianza kusanifu na kujenga mfumo huo.

Alisema mfumo huo utakuwa mbadala wa unaotumika kwa sasa wa TANePS na utatatua vikwazo kadhaa vya kiufundi na kukidhi mahitaji ya serikali katika sekta ya ununuzi nchini.

Aliongeza kuwa baadhi ya taasisi hizo ni TANROADS na TARURA ambazo zabuni zimeanza kutangazwa. Alibainisha kwa sasa wataanza na taasisi za ununuzi 101 kwa awamu ya kwanza itakayoanza na zilizobaki zitaanza kutumia Oktoba Mosi mwaka huu.

"Mfumo utaondoa mwingiliano wa kibinadamu na uamuzi wa kibinadamu, hivyo taasisi haitakuwa na uwezo wa kukwepa kutumia taratibu zilizopo na kuongeza uwazi na kufuata taratibu, uwajibikaji na mfumo umewekewa uwezo wa kufuatilia kila kinachotumika, mfumo utawachuja wote wazabuni wasiostahili," alisema.

Alisema mfumo utaondoa tatizo la wazabuni kushawishi wanapoomba kazi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakimu Maswi, alisema kila kitu kitafanyika ndani ya mfumo ikiwamo saini na kuondoa mwingiliano wa kibinadamu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - MWANZA**
**SHAURI NA. 449 LA 2022**
**1. ANDREW HEZRON LAZALO**
**2. HELENA JOHN MWASALEMBA.........MDAI**
**DHIDI YA**
**1. SAMSON WILLIAM WALWA**
**2. EVODIUS MWANGA HENGA........WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

KWA: SAMSON WILLIAM WALWA & EVODIUS MWANGA HENGA
MNAFAHAMISHWA KWAMBA WALETA MAOMBI HAPO JUU AMEFUNGUA SHAURI DHIDI YENU KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MKOA WA MWANZA, OMBI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA TAREHE 27/06/2023 KATIKA CHUMBA CHA BARAZA, BARABARA YA MAKONGORO, JENGO LIKO MKABALA NA MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA MJINI.
KWA HIVYO MNATAKIWA KUHUDHURIA KATIKA BARAZA SIKU HIYO NYIE WENYEWE , WAKILI WENU AU MTU MWINGINE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUJIBU OMBI HILO.
KAA- MKIJUA KUSHINDWA KUFIKA BARAZA LITASIKILIZA OMBI HILO NA KUTOA UAMUZI BILA NYINYI KUWEPO.
IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA BARAZA LEO TAREHE 19/06/2023

MAYEYE S. M
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MWANZA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

**KUONGEZWA KWA MUDA WA KUTUMA MAOMBI MAPYA NA UPANDISHAJI DARAJA WA LESENI ZA MAUDHUI (UTANGAZAJI WA KIBIASHARA – REDIO) KUTOKA TAREHE 25 JUNI 2023 MPAKA TAREHE 9 JULAI 2023 KWA MAENEO YALIYOAINISHWA HAPA CHINI**

1. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na.12 ya mwaka 2003 yenye jukumu la kusimamia huduma za mawasiliano ya Kielektroni na Posta nchini Tanzania.

2. Kwa mujibu wa Kanuni za Taratibu za Utoaji Leseni, Tangazo la Serikali Na.422 la mwaka 2014, TCRA imeainisha Masafa kwa ajili ya utoaji wa Huduma za Maudhui. Hivyo dirisha la maombi ya leseni ya utoaji wa huduma za maudhui ya redio limefunguliwa katika maeneo yafuatayo:-

| Mkoa | Eneo la Huduma | Kiasi cha Masafa Yaliyopo |
|---|---|---|
| Mwanza | Mwanza | 2 |
| Morogoro | Morogoro | 1 |
| Njombe | Njombe | 2 |
| | Ludewa | 2 |
| | Wanging'ombe | 2 |
| | Makete | 2 |
| | Makambako | 2 |
| Kagera | Kyerwa | 1 |
| Kigoma | Buhigwe | 1 |
| | Kigoma | 1 |
| | Kasulu | 3 |
| Geita | Mji wa Geita | 1 |
| | Chato | 1 |
| | Bukombe | 1 |
| Shinyanga | Mji wa Kahama | 1 |
| | Kishapu | 2 |
| | Manispaa ya Shinyanga | 1 |
| Simiyu | Bariadi | 2 |
| | Busega | 2 |
| | Itilima | 2 |
| Mtwara | Mtwara | 2 |
| | Masasi | 2 |
| | Tandahimba | 2 |
| | Newala | 2 |
| Singida | Manispaa ya Singida | 2 |
| | Manyoni | 1 |
| | Ikungi | 1 |
| | Mkalama | 1 |
| | Iramba | 1 |
| Rukwa | Manispaa ya Sumbawanga | 2 |
| | Sumbawanga Vijijini | 2 |
| | Kalambo | 2 |
| | Nkasi | 2 |
| Manyara | Hanang | 2 |
| | Kiteto | 2 |
| | Mbulu | 2 |
| | Simanjiro | 2 |
| Ruvuma | Mbinga | 1 |
| | Nyasa | 1 |
| | Tunduru | 1 |
| | Manispaa ya Songea | 2 |
| | Manispaa ya | 1 |
| Lindi | Nachingwea | 1 |
| | Kilwa | 1 |
| | Mtama | 1 |
| | Liwale | 1 |
| | Mji wa Lindi | 2 |
| | Ruangwa | 2 |
| Tanga | Tanga | 1 |
| Mara | Mji wa Musoma | 1 |
| | Rorya | 1 |
| | Mugumu | 2 |
| | Tarime | 1 |
| Iringa | Manispaa ya Iringa | 1 |
| | Kilolo | 1 |
| | Mafinga (Mufindi) | 1 |
| Tabora | Manispaa ya Tabora | 2 |
| | Igunga | 1 |
| | Kaliua | 1 |
| | Urambo | 1 |
| | Nzega | 1 |
| Katavi | Mpanda | 2 |
| | Nsimbo | 2 |
| | Tanganyika | 2 |
| | Mlele | 2 |

3. Waombaji wanatakiwa kuzingatia mwongozo wa uwasilishaji wa maombi unaopatikana katika tovuti ya TCRA: **www.tcra.go.tz.**
4. Maombi yote ya utoaji wa huduma tajwa hapo juu yawasilishwe kwa kupitia mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao Tanzanite Portal kupitia kiunganishi kifuatacho: **https://tanzanite.tcra.go.tz/index.htm** kabla ama ifikapo tarehe 9 Julai, 2023.
5. Tafadhali zingatia kwamba, endapo waombaji katika eneo fulani la huduma wako wengi zaidi ya kiasi cha Masafa yaliyoainishwa katika eneo hilo, TCRA itaweka Masafa ya eneo husia katika mchakato wa ushindani, yaani zabuni / Mnada.
6. Waombaji watakaoingia kwenye mchakato wa ushindani wa zabuni au mnada watajulishwa ili waweze kuwasilisha zabuni zao katika bahasha iliyofungwa ambayo itafunguliwa mbele ya wazabuni wote.

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Mawasilaino Tanzania,**
**Mawasiliano Towers,**
**20 Barabara ya Sam Nujoma,**
**S. L. P. 474,**
**14414 DAR ES SALAAM.**



# TAKUKURU yaagizwa kuchunguza tuhuma upotevu saruji

**Na Mary Mosha**, ROMBO

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru, Abdala Shaib Kaim, ametoa siku nne kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, kufanya uchunguzi wa madai ya upotevu wa mifuko 97 ya saruji katika Zahanati ya Msangai iliyoko wilayani humo.

Zahanati hiyo ilijengwa mwaka 2017 kwa michango ya wananchi kutokana na umuhimu kwa jamii na serikali ilitoa Sh. milioni 195 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la zahanati hiyo, choo cha nje, kichomea taka pamoja na uzio kuzunguka eneo hilo.

Agizo hilo lilitolewa juzi baada ya Mwenge wa Uhuru kufanya uchunguzi na kubaini kutokuwapo kwa matumizi sahihi ya mifuko hiyo, jambo ambalo ni ukiukwaji wa utaratibu.

"Uchunguzi wa kitaalamu tuliofanya kwenye nyaraka haionyeshi mifuko 97 ya saruji, tunawaagiza TAKUKURU kuhakikisha wanafanya uchunguzi wa kina na ikiwa kuna ubadhirifu wowote hatua za kisheria zichukuliwe," alisema.

Akisoma taarifa kwa viongozi wa Mwenge wa Uhuru, Mganga Mkuu wa Wilaya Rombo, Deogratias Maruba, alisema mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2018 ambapo na shughuli zote zilizofanyika zimegharimu Sh. milioni 112.4 ikijumuisha ununuzi wa eneo la ujenzi kwa kiasi Sh. milioni 13.

"Shughuli ambazo bado hazijafanyika ni kuweka sakafu, kuweka mfumo wa umeme awamu ya pili, kuweka mfumo wa maji awamu ya pili, kuchimba mashimo ya choo, kujenga choo cha nje, kujenga kichomea taka pamoja na uzio kuzunguka eneo la zahanati na imegharimu Sh. milioni 95.5," alisema.

Kadhalika kiongozi huyo, alitoa siku tatu kwa Halmashauri ya Rombo, kuhakikisha wanafanya marekebisho ya baadhi ya mapungufu yaliyoonekana ikiwamo mradi wa vyoo katika Shule ya Sekondari Horombo.

"Halmashauri fanyeni maboresho ya upungufu uliojitokeza kwenye mradi, pia kwenye mradi wa maji wa lita 500 licha ya mradi huo kukamilika lakini natoa mwezi mmoja na nusu kuhakikisha mnafanya tathimini ya uharibifu wa mazingira," aliongeza.



Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema (kulia), akimkabidhi kishikwambi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Handeni, Mariamu Ukwaju (kushoto), ambavyo vimetolewa kwa ajili ya wakurugenzi wa halmashauri 11 za mkoani humo na Shirika la Viwango nchini (TBS) juzi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# TRA: Hatutafunga biashara ya mtu yeyote

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesema haitafunga maduka wala biashara ya mfanyabiashara yeyote kwa kuwa huo ndio utaratibu waliojiwekea.

Kadhalika imesema ikitokea kama kuna mtu yeyote amejitambulisha kuwa ni mfanyakazi wa TRA mfanyabiashara anapaswa kuomba utambulisho wake ikiwamo kumwonyesha kitambulisho. Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa TRA, Rachel Mkunday, wakati akizungumza katika semina maalumu kwa waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Arusha (APC).

"Kwa sasa TRA haihusiki kufunga biashara au maduka ya mfanyabiashara yeyote na ikitokea mtu amejitambulisha kuwa ni mtumishi anayetoka katika ofisi yetu mwombe akupe kitambulisho cha kazi ili kumtambua," alisema Rachel.

Naye Meneja wa TRA Mkoa wa Arusha, Eva Raphael, alisema mamlaka hiyo itaweka mifumo rahisi ya kulipa kodi kwa kuboresha miundombinu na kutoa elimu ya mlipakodi kwa kuwa huo ndio mpango mkakati wao kwa sasa. "Waandishi mmekuwa mkono wa tatu kwetu kwa kutoa taarifa kwa wananchi mambo tunayofanya na ninaahidi tutaendelea kushirikiana kwa kufanya kazi pamoja ikiwamo kutoa elimu kwa umma," alisema.

Alisema ulipaji wa kodi ni takwa la kisheria kwa kila mwananchi na fedha zinazopatikana zinatumika kwenda kutoa huduma mbalimbali katika jamii.

"Kulipa kodi ni jambo muhimu sana kwa kuwa inasaidia kupeleka huduma kwa wananchi ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji, shule, hospitali, umeme pamoja na kuendesha serikali na taasisi za umma.

Hata hivyo, alisema taasisi hiyo ya umma ina wajibu wa kutoa elimu ili kila mtanzania kufahamu wajibu na haki kwenye nchi na taifa lake.

"Waandishi wa habari ni kisemeo cha serikali kwa kufikisha kwa kufikisha taarifa sahihi kwa wananchi hivyo nawashukuru kwa kuwa mmekuwa wadau muhimu tunaoshiriki katika utendaji kazi kwa ajili ya ujenzi wa taifa letu," alisema.

# Wadau madini waomba huduma ya hospitali

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WADAU wa madini ya tanzanite katika Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara wameiomba serikali kusaidia kujenga hospitali, kituo cha afya au zahanati kwa kuwa eneo la machimbo hayo hakuna vituo vya huduma za afya.

Walisema kutokana na serikali kukusanya fedha nyingi kupitia kodi inayopatikana kwenye madini ya tanzanite, kunatakiwa kuwekezwa kwa huduma za afya kwa manufaa ya wadau wote wa madini hayo.

Wakizungumza jana wadau hao akiwamo, Fatuma Kifunta, alisema serikali inakusanya fedha nyingi kupitia kodi ya madini ya tanzanite, hivyo serikali inapaswa kurudisha kwa jamii kwa kujenga zahanati, kituo cha afya au hospitali.

Naye Tausi Bakari, alisema serikali inawajibu wa kuweka miundombinu rafiki kwenye machimbo hayo ikiwemo kutengeneza barabara zilizoko ndani ya ukuta unayozunguka migodi.


"Barabara ni mbovu, watu wanatumia pikipiki hakuna magari ya abiria, hakuna maji hivyo tunaiomba serikali ivute maji kwenye machimbo kwa kuwa haya yanayopelekwa na magari yanauzwa kwa bei ghali," alisema.

Mwanasheria wa shirika lisilokuwa la kiserikali la Civil Social Protection Foundation (CSP), Eliakim Paulo, alisema waliandaa kongamano la mradi wa tanzanite kwa uchumi imara wa mwanamke kwa kuwahusisha wanawake wadau wa madini hayo, wasaidizi wa kisheria na waandishi wa habari.

Paulo alisema mradi wa tanzanite, kwa uchumi imara wa mwanamke unahusisha wanawake wajasiriamali wa madini hayo wa kata za Mirerani, Endiamtu na Naisinyai wanaofanya biashara zao ndani ya ukuta unayozunguka migodi ya madini hayo.

"Lengo ni uchechemuzi kwenye kongamano hili na pia waandishi wa habari wataingia ndani ya ukuta unaozunguka migodi ili kuangalia changamoto na mafanikio ya wanawake hao," alisema.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Mirerani (TEO), Isack Mgaya, akifungua kongamano hilo lililofanyika kwa siku nne aliipongeza CSP kwa kuanzisha mradi huo kwa uchumi imara wa mwanamke.





## W'biashara wakumbushwa matumizi ya teknolojia

**Na Waandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wa mikoa ya Kanda ya Ziwa wameshauriwa kuongeza juhudi, ujuzi katika biashara kwa kuendana na mabadiliko ya dunia kupitia matumizi ya teknolojia katika kujipatia masoko ndani na nje ya nchi.

Hayo yalibainishwa kwa nyakati tofauti na wadau wa biashara nchini katika makongamano ya biashara yaliyofanyika katika Mkoa wa Mwanza na Kagera yakiwakusanya kwa pamoja wafanyabiashara wakubwa na wadogo lengo likiwa ni kutoa elimu na fursa za kufanya biashara kwa tija.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Mwanza, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Charles Shirima, alisema kuwa kupitia jukwaa hilo vijana wataweza kuanzisha majukwaa katika biashara zao na zile watakazozianzisha.

Alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kuhakikisha vijana wanapata uelewa wa fedha ambao utawasaidia kujiajiri, kujikwamua kiuchumi na kukuza mitaji yao.

Alisema kuwa miongozo ya mitaji ya alaiki ni mfumo unaotumia TEHAMA ambayo inawezesha biashara ndogo na za kati kukusanya fedha kutoka kwa umma kwa ajili ya kuwekeza.

"Biashara ndogo na za kati zinakuwa hazina sifa za kuorodheshwa kwenye soko la mitaji au mikopo kutoka benki kwa hiyo mitaji ya alaiki ni jukwaa linalowezesha biashara hizo kupata fursa ya kukusanya mitaji kutoka kwa umma," alisema Shirima.

Ofisa Mipango na Fedha kutoka Shirika la SIDO Mkoa wa Mwanza, Salum Msengi, alisema vijana ambao wamehudhuria mafunzo hayo watakuwa mfano kwa vijana wengine katika jamii kwa kutunisha mifuko ya hisa kupitia wao kwa wao.

Katika hatua nyingine kongamano kama hilo lilifanyika mkoani Kagera likiwaunganisha wafanyabiashara kutoka katika nchini za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Burundi na Tanzania.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Spact Co Ltd, Alden Kilaja, alisema lengo la kuunganisha wafanyabiashara hao ni kufanya ushirikiano wa kuingiza na kutoa bidhaa katika nchi hizo.

"Haya maonyesho yanalenga kuimarisha azma ile ya nchi uanachama kufanya biashara kwa kupitia Soko la Afrika Mashariki ikilinganishwa hapa mkoani kwetu Kagera tunavitu vingi mbavyo vikichangamkiwa kama fursa vitaongeza uchumi na kutangaza nchi," alisema Kilaja. Alisema ushiriki utafanya kuwapo na wafanyabiashara watakaotumia teknolojia ya kibiashara na kuingizwa kwenye mifumo ya kitakwimu na kuongeza uchumi.

Mshikiri wa maonyesho hayo kutoka Taasisi ya Nitetete Foundation, Dk. Frola Lauo, alisema ushirikiano huleta umoja na ufahamu wa upungufu unaofanywa na wafanyabishara kupitia bidhaa zinazozalishwa. Mfanyabiashara wa vinywaji kutoka DRC, Ambroise Rissasi, alisema huwa anakuja Tanzania kufanya uzoefu wa kubadilishana mawazo kwani vitu vingine hutoka nchini kwenda DRC hupendwa na kutumika zaidi.

**Imeandaliwa na Vitus Audax (MWANZA), Restuta Damian (BUKOBA).**

# Wakosa huduma ya 'ambulance' zaidi ya miaka 5

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WAKAZI wa Kisiwa cha Juma kilichopo wilayani Sengerema mkoani Mwanza wameiomba serikali kupeleka boti ya kubeba wagonjwa kutoka kisiwani humo baada ya kukosa huduma hiyo kwa zaidi ya miaka mitano.

Wamesema hali hiyo imesababishwa na boti iliyokuwapo kuharibika na kuleta adha ya usafirisha kwa wagonjwa.

Inaelezwa kuwa mama wajawazito, watoto pamoja na wagonjwa wengine hushindwa kupata huduma kwa wakati, kwamba kulazimika kupanda mitumbwi inayotumia muda mrefu kufika katika Kituo cha Afya Sengerema.

Diwani wa Kata ya Katunguru, Sadick Jimola, alisema kuwa ni wakati wa serikali kuingilia kati suala hilo ili kuwanusuru wakazi wa kisiwani humo kuweza kupata huduma kwa wakati.

"Baadhi ya wananchi wamekuwa wakipoteza maisha pindi wakipelekwa kwenye huduma kupitia usafiri wa mitumbwi ambayo imekuwa ikiwachelewesha kufika sehemu za kupata huduma kwa wakati," alieleza wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani kilichoketi juzi kujadili ripoti ya CAG.

Akizungumza katika kikao hicho kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Katibu Tawala wa mkoa huo, Elikana Balandya aliiagiza halmashauri hiyo kufanya tathmini ya matengenezo ya boti ili wananchi warejeshewe huduma kama ilivyokuwa awali.

Alisema halmashauri inatakiwa kutengeneza boti hiyo ya wagonjwa haraka iwezekanavyo kabla ya mwaka wa fedha kuisha kwani hakuna ambacho kinakwamisha isipokuwa ni kutokuwa makini na kazi.

Alisema haiwezekani tangu mwaka 2019 hadi leo wananchi hawana boti hali inayo hatarisha maisha yao.



Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, wakiwa kwenye kikao maalumu cha baraza juzi, kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha (2021/2022), ziliibuliwa hoja 54 na kujibiwa 24 huku 30 zikisalia na kuendelea kutafutiwa viambatanisho vya nyaraka muhimu ili kuzifuta. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Shinyanga yapokea bil.345/- usambazaji umeme vijijini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amesema mkoa huo umepokea Sh. bilioni 345 kwa ajili ya usambazaji wa huduma ya nishati ya umeme vijijini (REA) ikiwamo kuanzisha mradi mkubwa wa kuzalishaji umeme jua megawati 150 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu.

Mndeme aliyabainisha hayo juzi katika mkutano maalum wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Msalala lililoketi kujadili na kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kusema kuwa nishati hiyo itaongeza nguvu katika viwanda na uzalishaji utaongezeka sambamba na kuongeza ajira kwa vijana.

Alisema kati ya hizo Sh. bilioni 345 za usambazaji wa nishati ya umeme vijijini Sh. bilioni 275 zinatumika kuanzisha mradi huo mkubwa wenye megawati 150 na kwa kuanzia mradi huo utazalisha megwati 50. Aliongeza kuwa megawati 150 zitaingizwa kwenye gridi ya umeme wa taifa na kuongeza nguvu katika viwanda na uzalishaji utaongezeka, hivyo kuwataka wenye uwezo wa kuwekeza wawekeze katika viwanda kwa sababu siku za baadaye kutakuwa na nishati ya umeme wa uhakika.

Katika hatua nyingine, Mndeme alisema wamepokea Sh. bilioni 14 kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji kutokana na ukosefu wa mvua katika misimu miwili ya kilimo iliyopita, hivyo kila diwani kwenye eneo lake ahakikishe anahamasisha wananchi kulima mazao ya chakula na biashara.

Alisema, serikali kupitia Wizara ya Kilimo imekuwa ikitengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya wakulima wake ikiwamo kupunguza gharama za pembejeo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kati ya hizo Sh. bilioni 1.4 zimetolewa katika Halmashauri ya Msalala kuanzisha kilimo cha umwagiliaji Chela. "Maofisa ugani wetu hakikisheni mnawatembelea wakulima mara kwa mara na kutoa elimu ya kulima kisasa kulingana na hali ya maeneo yao ya kilimo, tunataka msimu ujao tuongoze kwa uzalishaji nchi nzima," alisema Mndeme.

Diwani wa Ikinda, Matrida Musoma, alisema watashirikiana na maaofisa ugani wa kata kuhakikisha wanawahamasisha wananchi wao kulima kwa tija kulingana na hali ya maeneo yao ili kupata mavuno mengi ya chakula na biashara kupitia mikutano ya hadhara wanayoifanya.

Nipashe
Spotika



MAKIPA WA5 WA KUMRITHI DAVID DE GEA MAN UTD 12 - 13




# VIUNGO WA4 WANAOWEZA KUWA SAHIHI PALE ARSENAL

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal kwa muda mrefu imemchukulia Declan Rice kama lengo lao kuu kwenye safu ya kiungo wa kati msimu huu wa majira ya joto, na ni kwa sababu nzuri tu.

Nahodha huyo wa West Ham anaonekana kumaliza muda wake wa kukaa kule London Mashariki kwa kiwango cha juu zaidi baada ya kuiongoza kutwaa ubingwa wa Ligi ya Europa Conference mjini Prague.

Alfajiri mpya inamngoja kiungo huyo wa kati na Arsenal wanaonekana kama waliopewa nafasi kubwa ya kumsajili nyota huyo wa Kimataifa wa England.

Taarifa kuhusu mustakabali wa Rice zote zilionesha mwelekeo mzuri kwa Arsenal licha ya kwamba ofa mbili za awali zilikataliwa.

Ilionekana kama suala la muda kabla ya makubaliano kufikiwa, lakini kuondoka kwa Ilkay Gundogan kule Manchester City kuelekea Barcelona kumebadili mwelekeo wa mbio hizo.

Man City sasa wako vizuri na wanahusika kikweli katika kuitaka saini ya Rice huku wakitayarisha ofa nono.

Mashabiki wa Arsenal tayari waliona kwamba, Rice ni mali yao na atakuwa kwenye jezi zao msimu wa 2023/24 na zaidi.

Lakini kujitokeza kwa Man City kwenye mbio hizo kumebadilisha upepo.

Makala haya inawaangalia viungo wanne ambao wanaweza kufiti zaidi pale Arsenal kama ikishindwa kumnasa Rice...

**#1. Joao Palhinha**

Marekebisho ya safu ya kiungo ya Arsenal yanatarajiwa kuwafanya Granit Xhaka na Thomas Partey kuondoka na Rice alionekana kama chaguo kwa nafasi ya namba sita na pia kucheza namba nane kwenye mfumo wa kocha Mikel Arteta.

Kwa hiyo uingizwaji unaowezekana hutofautiana katika wasifu, ingawa uchangamato na uwezo wa kutekeleza majukumu yote mawili itakuwa bora. Arsenal wanaweza kurejea kwa Moises Caicedo ikiwa City itamsajili Rice, wakati Romeo Lavia ni kipaji cha kiungo ambacho wangependa kukileta pamoja na Rice au yeyote yule.

West Ham wanamlenga Palhinha wa Fulham kama mbadala wa Rice na 'Washikabunduki' huenda wakatamani kumsajili kutokana na msimu wake mzuri wa kwanza kwenye Ligi Kuu.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ureno ana masuala ya kinidhamu, lakini yeye ni mshindi mkubwa wa mpira na msomaji wa mchezo, huku akiwa na uwezo mkubwa wa kumiliki mpira. Atakuwa chaguo bora kwa nafasi ya namba sita, na Arsenal italazimika kulipa karibu pauni milioni 90.

**#2. Kalvin Phillips**

Baada ya kuwa na wakati mzuri kule Leeds United na England, Phillips alipata uhamisho wa kwenda Manchester City msimu uliopita wa majira ya joto, lakini msimu wake wa kwanza ulimshuhudia akikosa namba mbele ya Rodri.

Alitumia dakika 593 kucheza katika mashindano yote, lakini kiungo huyo wa kati amesema anataka kubaki Etihad na kupigania nafasi yake.

Hata hivyo, hatua ya Rice, hata baada ya kuondoka kwa Gundogan, inatia shaka zaidi juu ya mustakabali wa Phillips. Kumwondoa Rodri kwenye chati ya kina imethibitika kuwa haiwezekani hadi sasa na Pep Guardiola anaweza kutumani Rice kama mbadala wa Mhispania huyo na Mateo Kovacic ambaye anaweza kutumika mbele zaidi - ambapo Rice atacheza zaidi.

Klabu kadhaa za Ligi Kuu England zinavutiwa na Phillips msimu huu wa majira ya joto na Arsenal wanaweza kujiunga katika kinyang'anyiro hicho iwapo watahitaji kutafuta mbadala mpya.

**#3. Khéphren Thuram**

Inaonekana Liverpool wamekamilisha mpango huu, lakini kunaweza kuwa na wakati kwa 'Washikabunduki' kunyakua dau la kwanza la 'Wekundu' hao ambalo halijawekwa wazi hadi sasa.

Thuram amepata sifa nyingi kutokana na uchezaji wake akiwa Nice, huku Liverpool wakimtaja kuwa mchezaji anayefuata katika safu ya kiungo baada ya kumsajili Alexis Mac Allister kutoka Brighton.

Kijana huyo wa Kifaransa anayeweza kutumia vitu vingi ambaye anasimama nje kutokana na mtazamo wa kimwili. Ana urefu wa futi sita na ni mgumu sana kumnyang'anya mpira, huku uwezo wake wa kumiliki mpira ukiwa ni sifa kuu. Muhimu zaidi, ana uwezo wa kucheza kama namba sita na nane kwani anafurahia kupokea mpira na zaidi katika awamu ya kujenga.

Arsenal haitakuwa na budi kuvunja benki ili kumsajili Thuram pia. Ofa ya kwanza ya Liverpool inatarajiwa kuwa pauni milioni 40.

**#4. Amadou Onana**

Haukuwa msimu rahisi zaidi wa Ligi Kuu England kwa Onana, ambaye alikuwa sehemu ya timu mbaya ya Everton, lakini Mbelgiji huyo alionekana kuwa mmoja wa taa za 'Toffees' hao.


Ikiwa Arsenal wanataka kuizidi Man City msimu ujao, lazima wajiongezee nguvu na Onana ni mtu wa muhimu kwao. Kiungo huyo mahiri ana nguvu na Arteta aliona unyama wa Onana wakati Everton walipoichapa Arsenal bao 1-0 pale kwenye dimba la Goodison Park katika kipindi cha pili cha msimu.

Mbelgiji huyo ni mchezaji halisi wa sanduku kwa sanduku ambaye uwezo wake wa angani ni tishio katika tatu ya mwisho. Arsenal wamekuwa wakihusishwa na kutaka kumsajili.

Onana anaweza kufanya kazi vizuri kama mtekelezaji wa safu ya kati upande wa kushoto wa safu ya kiungo ya Arsenal.

## ISIKUPITE

ENDAPO Kocha wa Juventus, Massimiliano Allegri atakubali ofa ya euro milioni 120 aliyopewa na Klabu ya Al-Hilal ya Saudi Arabia. Atakuwa ndiye kocha anayelipwa zaidi katika historia ya soka duniani.



# MAKIPA WA5 WA KUMRITHI DAVID DE GEA MAN UTD




David de Gea

**MANCHESTER, England**

BAADA ya miaka 11 ya utumishi wa golikipa, David de Gea, ndani ya Manchester United unaweza kuwa unakaribia mwisho.

Alipotua hapo kwa 'Mashetani Wekundu', Mhispania huyo alichanua haraka na kuwa mmoja wa magolikipa bora zaidi duniani na aliwindwa na Real Madrid kabla ya kumnasa Thibaut Courtois. De Gea ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu Ligi England.

Licha ya kupata tuzo za Golden Glove msimu wa 2022/23, mustakabali wa De Gea ndani ya Man United hauonekani huku mkataba wake ukielekea ukingoni.

Klabu hiyo ina chaguo la kuongeza mkataba wake kwa miezi 12 zaidi, lakini kwa hali ilivyo hali ya kipa huyo wa United ni tete na ambayo inaweza kubadilika mara moja.

Mashetani Wekundu wanaweza kushikamana na De Gea, lakini anakabiliwa na makosa na wanaweza kumruhusu Mhispania huyo kuondoka ili kupendelea mbadala mdogo na wa kisasa zaidi kwa ustadi uliowekwa, unaofaa zaidi kwa kocha Erik ten Hag.

Makala haya inawangalia magolikipa watano ambao wanaweza kuchukua nafasi ya De Gea pale Man United msimu huu wa majira ya joto.

### #1. Diogo Costa

Golikipa namba moja wa Ureno amekuwa akiwaniwa na Man United kwa muda mrefu na anachukuliwa kuwa mmoja wa walengwa wakuu wa klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto.

Hata hivyo, Costa mwenyewe amepuuza uvumi wa kuhamia Old Trafford na kusema anataka kuendelea na Porto, klabu ya "maisha" yake msimu ujao na zaidi.

Lakini Mashetani Wekundu wanamtaka kwa udi na uvumba na wanaripotiwa kujaribu kupunguza bei inayotakiwa na Porto, inayoaminika kuwa karibu pauni milioni 64.

Costa, mpiga shuti bora ambaye humiliki mpira kwa urahisi na ustadi wa kufagia nje ya eneo la hatari, alicheza mechi 16 bila kuruhusu bao kwenye Ligi Kuu Ureno msimu uliopita.

### #2. David Raya

Huku ukiwa umesalia mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake na Brentford, 'Nyuki' hao wamemwambia Raya kwamba anaweza kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto na Tottenham Hotspur imepiga hatua katika kumsaka Mhispania huyo. Lakini bei ya Brentford ya pauni milioni 40 kwa sasa ni kikwazo.

Man United pia inataka kumnunua Raya, ambaye alikuwa mmoja wa makipa waliofanya vema kwenye Ligi Kuu England msimu wa 2022/23.

Mchanganyiko wa Raya wa kuhimili mashuti na kazi ya ustadi akiwa na mpira miguuni mwake, inamfanya kuwa kitu cha kuhitajika kwa klabu kadhaa, na United wanapaswa kufikiria kuwapiku Tottenham katika mbio za kuwania saini yake iwapo Spurs wataendelea kujikwaa katika mazungumzo.

### #3. Jordan Pickford

Pickford alijijengea heshima kutokana na uchezaji wake bora kwa England kwenye mashindano makubwa. Ni mara chache ameweka mguu vibaya kwa 'Simba Watatu' (Timu ya Taifa ya England).

Kiwango chake akiwa na Everton katika miaka ya hivi karibuni kimekuwa cha kusuasua zaidi, lakini alifurahia msimu mzuri akiwa na 'Toffees' hao na hatimaye akacheza jukumu muhimu katika kusalia kwao Ligi Kuu England.

Pickford, ambaye anajivunia upigaji pasi wa kuvutia, lakini uwezo wake kwenye mpira umezidiwa kwa ujumla, ameibuka kama shabaha ya 'Mashetani Wekundu' msimu huu, na Ten Hag bila shaka akishangazwa na kiwango cha kuokoa hatari tisa cha Muingereza huyo dhidi ya timu yake Old Trafford Aprili.

### #4. Andre Onana

Onana alijitengenezea sifa nzuri chini ya kocha Ten Hag katika Klabu ya Ajax huku Mholanzi huyo akimtolea jicho kwa muda mrefu na sasa anaona kwamba anafaa kwenda kurithi mikoba ya De Gea.

Mpiga mashuti huyo wa Cameroon, ametambulishwa kama kipa bora wa siku hizi, ambaye anacheza kwa umaridadi na ustadi wa kipekee licha ya uchezaji wake usio na maelewano na wa zamani.

Marufuku ya matumizi ya dawa za kuongeza nguvu ilizuia maendeleo yake kwa kiasi fulani, lakini msimu wa 2022/23 ulikuwa bora kwa Onana alipomnyakua Samir Handanovic kati ya vijiti vya Inter kabla ya kuchukua jukumu muhimu katika kupaa kwa 'Nerazzurri' mwisho wa msimu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, aliandikisha pasi nyingi zaidi (nane) na kuokoa hatari 48 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya huku, Inter wakifungwa kwenye fainali na Manchester City.

### #5. Mike Maignan

Wachache sana walidhani kwamba wakati AC Milan ilipoachana na Gigi Donnarumma, ambaye inaaminika kuwa ujio wa pili wa Gigi Buffon, kungekuwa na tatizo kubwa pale kwenye kikosi hicho.

Lakini Rossoneri walifanya hivyo hasa na kipa wa zamani wa Lille, Maignan, ambaye kiwango chake cha ajabu kilisaidia Milan kushinda Scudetto (Kombe la Ligi Kuu Italia) msimu wa 2021/22.

Kazi bora ya Mfaransa huyo katika kumiliki mpira ikilinganishwa na Donnarumma iliongeza mwelekeo mpya kwa upande wa kocha Stefano Pioli, huku uthabiti wake wa ajabu ukifanya makosa kuwa nadra.


Kupanda kwake kunapaswa kumwona akiibuka kama namba moja wa Ufaransa baada ya kustaafu kwa Hugo Lloris, na licha ya kukosa msimu wa 2022/23 kutokana na jeraha, Maignan ameonesha mara kwa mara ustadi wake. Kipa huyo mwenye umri wa miaka 27, anafaa kuwa mrithi kamili wa De Gea pale Manchester United.

## Nukuu


"Nina furaha sana. Kufikisha mechi 200 ni aina ya wakati ambao hutarajii kamwe. Ni mafanikio ya kushangaza. Na bila shaka kufunga bao la ushindi kunaifanya kuwa siku ya kipekee zaidi," **Cristiano Ronaldo baada ya kuwa mwanasoka wa kwanza kwa wanaume kucheza mechi 200 za kimataifa wakati wa ushindi wa Ureno wa kufuzu michuano ya euro 2024 dhidi ya Iceland Jumanne iliyopita.**



"Ukishindwa ukiwa Real Madrid, ni kama ulimwengu umekwisha, umesurubishwa. Unajisikia vibaya. Unarudi nyumbani na huna furaha," **Gareth Bale akielezea namna Lionel Messi atakuwa na presha ndogo ya kushinda katika Ligi Kuu Marekani (MLS), kwa sababu klabu za huko hazina presha.**



"Siku zote kuna ofa kutoka mahali pengine, lakini nimeamua kubaki kwa mwaka mmoja zaidi. Nina furaha sana na nina furaha ya kukaa hapa," **Nahodha wa Real Madrid, Nacho Fernandez baada ya kuongeza mkataba wa mwaka mmoja na klabu hiyo.**



# USAJILI NA TETESI KWA KLABU ZA LIGI KUU BARA



Kipa Mbrazili Caíque Luiz Santos da Purificacao, anayeichezea klabu ya Ypiranga Serie C nchini Brazil, ambaye yupo kwenye rada za Simba.

**Na Adam Fungamwango**

KLABU zote duniani sasa zipo kwenye pilikapilika za kusaka wachezaji watakaoviongezea nguvu vikosi vyao kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Klabu za Tanzania haziko nyuma, zimeanza harakati za kusaka wachezaji ndani na nje ya nchi ili ziwe imara msimu ujao.

Kuanzia bingwa mpaka timu zilizopanda daraja zipo kwenye hatua ya kuingia mikataba na wachezaji wapya, kabla ya nyaraka hizo baadaye kuzipeleka Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), pale zitakapohitajika, wakati dirisha kubwa la usajili linakapofunguliwa rasmi.

Baadhi ya klabu zimeshaanza kufanya usajili na kuwatambulisha rasmi, huku zingine zikiendelea na harakati hizo.

Kumekuwa na tetesi mbalimbali zikizihusisha klabu za Ligi Kuu na wachezaji kadhaa maarufu nchini na wale ambao si maarufu.

Katika makala haya tumekusanya baadhi ya taarifa za usajili na tetesi zake kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania.

**Kakolanya na Singida Fountaine Gate**

Golikipa Beno Kakolanya amesema amemaliza mkataba na Klabu ya Simba, na tetesi zinasema kuwa Beno huenda akajiunga na Singida Fountaine Gate FC ambayo imeipiku klabu moja kutoka Uarabuni.

Beno amesema aliipa nafasi ya kwanza Simba, lakini dau lao lilikuwa dogo, klabu ya Uarabuni ikaja na dau kubwa kidogo na kabla hajafanya chochote, klabu ambayo hakuitaja jina ikampa ofa nono zaidi.

**Sakho kutimkia Ubelgiji**

Winga wa Simba raia wa Senegal, Pape Sakho, huenda akatimkia Klabu ya K.V.C. Westerlo ya Ubelgiji.

Klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu nchini Ubelgiji, imetuma ofa ya dola 500,000, zaidi ya bilioni 1.1 za Kitanzania kwa ajili ya kumsajili winga huyo anayeichezea pia Timu ya Taifa ya Senegal, mkataba wake ukitajwa kuwa utaisha Juni 2024.

Awali, alikuwa anatakiwa kwa udi na uvumba na Klabu ya Azam huku mabosi wa 'Wekundu wa Msimbazi' wakiwa wamegawanyika, wakitaka kama ni kuuzwa basi auzwe nje ya nchi na si ndani.

**Morrison ni wa Singida Fountain Gate**

Baada ya Azam FC kukataa kuwa na mpango wa kumsajili aliyekuwa winga wa Yanga, Bernard Morrison, Klabu ya Singida Fountain Gate FC ipo kwenye nafasi kubwa ya kumsajili mchezaji huyo.

Morrison ambaye alipewa 'thank you', na Klabu ya Yanga hivi karibuni, klabu hiyo na Azam zilihusishwa, lakini Ofisa Mtendaji Mkuu, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema si mmoja wa wachezaji watakaowasajili.

**Beki wa Cotton Sports mbioni kutua Simba**

Klabu ya Cotton Sports ya Cameroon imekataa ofa iliyotumwa na Simba kwa ajili ya kutaka saini ya mlinzi Che Fondoh Malone.

Tetesi zinasema klabu hiyo inahitaji kiasi cha Sh. milioni 350 ili kumruhusu mlinzi huyo mkakamavu kujiunga na Simba.

**Yanga yasaka kiungo Asec**

Klabu ya Yanga ipo kwenye mazungumzo na Klabu ya Asec Mimosas ya Ivory Coastal kwa ajili ya kupata saini ya kiungo Mohamed Zoungrana raia wa nchi hiyo.

Hata hivyo, tetesi zinasema tayari Mabingwa wa Afrika, Al Ahly wameingilia dili hilo, hivyo kuwafanya Mabingwa wa Tanzania kupata upinzani.

Imeelezwa kama itamkosa basi inaweza kuangukia kwa Morice Chukwa, Mnaigeria anayeichezea klabu ya Akwa United.

**Mbrazil kushika mikoba ya Manula**

Klabu ya Simba ipo kwenye mazungumzo ya kukamilisha usajili wa golikipa raia wa Brazil, Caique Luiz Santos da Purificacao.

Klabu hiyo inahaha kusaka mbadala wa Aishi Manula aliyefanyia upasuaji hivi karibuni na anatarajiwa kukaa nje ya zaidi ya miezi minne.

Tetesi zinasema kuwa Simba iko kwenye nafasi nzuri kumpata kipa huyo mahiri baada ya Al Hilal kuwabania kumsajili kipa wao, Issa Fofana, huku kipa Mghana, Joseph Addo anayechezea Adiana Stars akiwekwa kiporo kama lolote likitokea.

**Muguna hatua moja kutua Namungo**

Baada ya kuachwa na Azam FC, kiungo raia wa Kenya, Kenneth Muguna, yupo katika hatua za mwisho kujiunga na Namungo.

Klabu hiyo tayari imeshamtangaza Erasto Nyoni ambaye siku chache zilizopita aliachwa na Simba.

**Mrithi wa Morrison Yanga huyu hapa**

Yanga inadaiwa ipo kwenye mazungumzo na Mkongomani Maxi Mpia Nzengeli, ili kuziba nafasi ya Bernard Morisson aliyeonyeshwa mlango wa kutokea.

Winga huyo anayeichezea Union Maniema, ameshawahi kuichezea Timu ya Taifa ya DR Congo, iliyoshiriki Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), msimu ulioisha.

**JE, WAJUA?**



Real Madrid (Hispania), Manchester City na Chelsea (England), Palmeiras (Brazil), Flamengo (Brazil), Monterrey (Mexico), Leon (Mexico), Al-Ahly (Misri), Wydad Casablanca (Morocco), Urawa Red Diamonds (Japan) na Al Hilal (Saudi Arabia), tayari zimefuzu kushiriki Kombe la Dunia la Klabu 2025 mwaka 2025 nchini Marekani litakaloshirikisha timu 32.



# Pentekoste 'kwachemka', Askofu Konki atakiwa kujiuzulu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAUMINI, wachungaji na viongozi wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania wamemtaka Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Peter Konki, kujiuzulu kwa kile walichodai kuwa ni kupoteza sifa ya kuwa kiongozi kutokana na kuvunja katiba ya kanisa.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana kwa nyakati tofauti baadhi ya waumini na wachungaji hao walisema hawana imani na kiongozi huyo kwa kuwa amepoteza sifa ya kuwa kiongozi wa kanisa lao. Mmoja wa viongozi wa kanisa hilo, Askofu Amos Maday, alisema tayari wameshamwandikia barua ya kumtaka kuachia nafasi hiyo ili aruhusu mkutano mkuu uitishwe na kiongozi mwingine achaguliwe na kuliponya kanisa.

"Sisi tulio orodhesha majina yetu nyuma ya barua hii ambayo ni wachungaji, waumini na viongozi mbalimbali wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania tunakufahamisha kuwa tumekosa imani na wewe na tunakutaka ujiuzulu ili kuruhusu mkutano mkuu uitishwe na kiongozi mwingine achaguliwe kuliponya Kanisa," alisema.

Akizungumzia kuhusu vifungu vya katiba ya kanisa hilo alilovivunja kuwa ni Sura ya 9 Ibara ya 11 Kifungu Kidogo 3(a) 2 ambacho kinamtaka Askofu Mkuu akubalike ndani na nje ya kanisa ambapo kwa sasa yeye hana sifa hiyo tena.

Alisema kwa sasa askofu huyo hakubaliki ndani na nje ya kanisa na anachokifanya ni kusababisha migogoro.

"Katika uteuzi wa Katibu Mkuu wa Jimbo la Manyara Magharibi uliofanyiwa na Askofu Konki Aprili 13, 2023 ni uvunjifu wa Katiba Ibara ya 6 (iv) ambacho kifungu hicho kinaeleza katibu wa jimbo atachaguliwa na baraza la wachungaji na siyo kuteuliwa na Askofu Mkuu," alisema.

Askofu Maday alisema pia utawala wa kulipa kisasi wa Askofu Konki kwa wale asiowapenda umesababisha migogoro ndani ya kanisa na kupoteza makanisa na wachungaji wengine kujiunga katika makanisa mengine.

Alisema tuhuma nyingine ni askofu huyo kuondoa sura ya utaifa katika kanisa kwa kuwateua wajumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu (kamati tendaji) wote wa kabila lake jambo ambalo limeleta taswira mbaya na waumini kushindwa kuelewa nia yake ni ipi.

Mchungaji Daniel Diyame, alisema Askofu Konki amekuwa akitumia fedha za taasisi vibaya kwa kuwa hakuna kamati ya fedha na mipango ya kuidhinisha matumizi.

"Kwa muda wote wa uongozi wake kodi ya pango la vibanda 11 vya maduka yanayozunguka Kanisa la Babati Mjini haijulikani iliingia kwenye akaunti gani," alisema. Aidha, alisema tangu mwaka 2020 askofu huyo amekuwa akirekebisha katiba yeye mwenyewe na katibu wake bila kutumia vikao halali vya halmashauri kuu na mkutano mkuu jambo ambalo ndilo chanzo kikuu cha migogoro.

Alipotafutwa kutolea ufafanuzi kuhusu tuhuma hizo, Askofu Konki, alisema ameyapata malalamiko hayo kwenye mitandao ya kijamii na yeye hana cha kusema kwani hivi sasa jambo hilo lishafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Askofu Konki alisema: "Unataka kujua nini kama hilo la barua lipo tayari kwenye mitandao ya kijamii labda kama unalo jambo jipya kama hilo mimi sina cha kusema kwa kuwa hivi sasa tupo kwenye vyombo vya kisheria tayari tumeshatoka kwa msajili."



Mkuu wa Mauzo wa kampuni ya simu za mkononi wa Airtel Tanzania, Dodoma, Salum Ngululu (katikati), akikabidhi zawadi ya jokofu kwa mkazi wa Dodoma, Silvano Chigwaye ambaye ni mmoja wa washindi wa promosheni inayoendelea ya Upige Mwingi na Airtel katika hafla iliyofanyika mkoani humo mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu wa Mawasiliano wa Airtel Tanzania, Beatrice Singano. Ili kushiriki mteja wa Airtel anatakiwa kutumia huduma ama kufanya miamala ya Airtel money. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yatoa onyo kwa walimu wakuu, kamati za ujenzi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida, imewaonya walimu wakuu na kamati za ujenzi kwamba fedha za ujenzi wa miradi ya shule mpya za msingi siyo kwa ajili ya kulipana posho.

Kamanda wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Mzalendo Udege, alisema hayo katika mafunzo yaliyoandaliwa na ofisi yake yaliyowalenga walimu wakuu, madiwani, watendaji wa kata, wajumbe wa kamati za ujenzi za shule na mafundi wanaotekeleza mradi huo wa BOOST katika Manispaa ya Singida. Alisema walimu wakuu, kamati za shule na mafundi wahakikishe wanasimamia kwa umakini na uadilifu mkubwa ujenzi wa shule za msingi mpya zinazojengwa kupitia mradi wa BOOST.

"Tuzingatie uadilifu na uzalendo, fedha za mradi siyo za kulipana posho...tuwe na uchungu na miradi yetu kwani ni mali ya wananchi...tuache alama nzuri katika miradi tunayoisimamia," alisema.

Mzalendo alisema lengo la mafunzo hayo ni kwa ajili ya kupitishana katika mwongozo wa utekelezaji wa mradi wa BOOST, lakini walengwa wa mafunzo kuelezea changamoto wanazokutana nazo katika utekelezaji wa mradi na kuweza kuzitatua kwa pamoja.

Hivyo aliwataka washiriki hao kuzingatia sheria na taratibu za manunuzi ili kuepuka kusababisha hoja za ukaguzi na hivyo kuhimiza suala zima la uadilifu na uwazi. Alisema kamati zilizoundwa zishirikishwe kikamilifu na kila kamati iwajibike katika dhamana waliyopewa na kwa kufanya hivyo kutarahisisha mradi kutekelezeka kwa urahisi na kwa wakati.

Aidha, aliwataka washirikine na wahandisi kuhakikisha manunuzi yanaendana na mahitaji halisi ya vifaa, fundi aliyepatikana asiwe na zabuni ya kazi nyingi na usimamizi shirikishi kwa viongozi wa chama na serikali pamoja na wananchi ili kuwezesha utekelezaji wa mradi kulingana na muda.

Halmashauri ya Manispaa ya Singida imepokea zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa BOOST ambapo shule mpya mbili, madarasa manne ya awali, madarasa 15, matundu 13 ya vyoo vinajengwa kupitia mradi huo ambao unatarajia kukamilika Juni, 2023.

# SIDO yawapiga msasa vijana utengenezaji ngozi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Viwanda Vidogo nchini (SIDO) mkoani Dodoma kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), wametoa mafunzo ya kutengeneza ngozi kwa vijana 98 kutoka mikoa ya Tabora, Dar es Salaam na wenyeji Dodoma.

Lengo la mafunzo hayo ni pamoja na kuwaandaa vijana hao kwa ajili ya kujiajiri wao wenyewe ili waweze kujiinua kiuchumi wao na familia zao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Msimamizi wa kituo cha ngozi kutoka SIDO Dodoma, Stephano Ndunguru, alisema mafunzo hayo yamejumuisha vijana wa kike na kiume kutoka katika mikoa hiyo.

Alisema mafunzo haya ni muhimu kwa vijana kutokana na kwamba yanawasaidia kwenda kujiajiri wao wenyewe badala ya kusubiri kuajiriwa.

"Mafunzo haya ni muhimu sana kwa vijana kwa sababu yanawasaidia vijana kuondokana na dhana ya kuajiriwa badala yake wafikirie kujiajiri wao wenyewe," alisema Ndunguru.

Alifafanua zaidi ya kuwa mafunzo hayo ya wiki tatu yamewasaidia vijana kujua namna ya kutengeneza bidhaa za ngozi ambazo ni muhimu kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali kama viatu mikoba mikanda na bidhaa nyingine ambazo zinatumia ngozi kwa ajili ya kutengenezwa.

Kwa upande wake Ofisa Tarafa wa Wilaya, Zainabu Issa, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Dodoma aliwataka vijana hao kwenda kuzalisha bidhaa kwa pamoja ili kuweza kupata soko kubwa ndani na nje ya nchi.

Alisema wanapaswa kwenda kuyafanyia kazi mafunzo waliyopata ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora ambazo zitakuwa na uhakika wa soko.

Naye mwakilishi kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Santiel Mmbaga, aliwataka vijana kujiendeleza kielimu na kiufundi ili kuweza kufikia malengo yao waliokusudia kwenye ujasiriamali.

Alisema vijana wakiwa na ujuzi wao ni rahisi kwao kuweza kupanua wigo wa ujasiriamali wanaofanya ikiwamo ule waliopanga kuufanya baada ya mafunzo hayo.

Alifafanua zaidi ya kuwa vijana wanatakiwa kuchangamkia fursa za mafunzo pale zinapotolewa na taasisi mbalimbali hapa nchini.

Mmbaga alisema kuwa serikali kwa kushirikiana na wadau wamekuwa wakitoa fursa nyingi kwa vijana ili waweze kujiajiri.

Aliwataka vijana kuchangamkia fursa za mafunzo na mikopo inayotolewa na serikali ili kuendesha shughuli zao na kujiinua kiuchumi.





# Wananchi, TFS wavutana umiliki shamba la miti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO mpya wa ardhi unafukuta mkoani Mbeya kati ya wananchi wanaoishi kuzunguka shamba la miti la Kawetere na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) baada ya wakala huo kudaiwa kuvamia mashamba ya wananchi hao

Maofisa wa TFS wa shamba hilo wanadaiwa kuweka alama za mipaka mipya kwenye mashamba ya wananchi bila kuwashirikisha jambo ambalo wananchi hao wanadai kuwa wanataka kuporwa kwa nguvu maeneo yao.

Kata zinazoathirika na mgogoro huo ni Kata ya Nsalaga iliyopo katika Jiji la Mbeya na Kata ya Ruiwa iliyopo wilayani Mbarali ambapo zaidi ya wananchi 300 wa maeneo hayo wanaathirika na mpaka mpya.

Wakizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki wananchi hao walisema maeneo hayo ni ya kwao na wamekuwa wakiyatumia kwa muda mrefu kulima mazao mbalimbali yakiwamo mahindi na viazi mviringo.

Mmoja wa wananchi hao, Kenedy Mwelamla ambaye ni mkazi wa Kata ya Nsalaga alisema eneo ambalo TFS wameweka mipaka yao ni eneo ambalo ni muhimu kwa uchumi wao kutokana na kulitumia kwa kilimo.

Alisema mbali na mipaka hiyo kuwekwa, pia walipokea barua inayowataka waondoke kwenye maeneo hayo kwa maelezo kuwa eneo hilo ni sehemu ya shamba.

"Sisi haya maeneo tumekuwa tukiyatumia kwa muda mrefu, wengi tumezaliwa tumewakuta wazazi wetu wanalima, lakini sasa hivi tunaambiwa tuondoke bila kuambiwa kwa kwenda, tunaomba serikali itusaidie," alisema Mwelamla.

Naye Moses Kimbese alisema wameambiwa wavune haraka mazao yao na wasirudie tena kulima maeneo hayo jambo ambalo alisema linaharibu uhusiano baina yao na viongozi wa shamba hilo.

Alisema taarifa za kuwataka waondoke kwenye maeneo yao ni ya ghafla kwa maelezo kuwa hawakuwahi kuambiwa kwamba wataondoka ili wajiandae. "Mimi na familia yangu tupo tayari kuondoka kwenye maeneo haya ambayo wanayataka, lakini tunataka tujue tunakotakiwa kwenda kuishi na kufanya shughuli zetu," alisema Kimbesa.

Alisema wana watoto ambao wanawasomesha katika ngazi mbalimbali za elimu ikiwemo vyuo vikuu na kwamba chanzo cha fedha kinachowasaidia kuwasomesha watoto hao ni mazao wanayolima.

Naye Ponsio Chrispin ambaye ni mkazi wa Kata ya Ruiwa, alisema wananchi wanayo haki ya kumiliki ardhi na kuitumia kwa shughuli mbalimbali hivyo akaiomba serikali kutumia utaratibu mzuri wa kutanua maeneo yake.

Diwani wa Kata ya Nsalaga, Mchungaji David Ngogo, aliwataka wananchi kutotumia nguvu kudai haki zao na badala yake wanatakiwa kufuata sheria. Aliwataka kuwatumia vizuri viongozi wa maeneo yao kuwasilisha malalamiko yao ili wasaidiwe na kwamba wakitaka kutumia nguvu wanaweza wasifanikiwe.

Mhifadhi Mkuu wa shamba la miti la Kawetere, Arnold Shoo, alisema msitu huo ni muhimu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho hasa kwa kutunza mazingira na kwa uchumi wa taifa.

Alisema wamewapa muda wananchi waliolima mazao yao kwenye maeneo hayo wayaondoe na wasilime tena kwa maelezo kuwa shamba hilo ni muhimu.



Wakazi wa Kitongoji cha Mwashikamile wilayani Mbarali mkoani Mbeya wakiwasikiliza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii (hawapo pichani), walipotembelea eneo hilo mwishoni mwa wiki kuangalia mipaka mipya ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. **PICHA: NEBART MSIKWA**

## Wataalamu kilimo watakiwa kuwatembelea wakulima

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI mkoani Mbeya, imewataka wataalamu wa kilimo wa ngazi zote mkoani humo, kuwatembelea wakulima mashambani na kuwapa elimu ya mbinu bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Katibu Tawala wa mkoa huo, Rodrick Mpogoro, alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki wilayani Mbarali alipozungumza na wakulima wa skimu ya umwagiliaji ya Uturo ambayo ni miongoni mwa skimu zinazoboreshwa na serikali.

Aliwataka wataalamu hao kutumia maarifa waliyonayo kuhakikisha wanawasaidia wakulima kuongeza tija kwenye uzalishaji ili kukuza uchumi pamoja na kuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula.

Vilevile aliwataka wataalamu hao kuwaelimisha wakulima kuhusu utunzaji wa mazingira ili kilimo wanachofanya kiwe endelevu kwa kuhakikisha maji yanaendelea kuwapo na mvua inanyesha ya kutosha.

"Wewe umesomea kilimo na umeajiriwa na serikali kwa ajili ya kuwasaidia wakulima lakini muda wote unakaa ofisini kufanya nini? Sasa kuanzia leo wataalamu wote wa sekta hii kazi yenu ni mashambani kwa wakulima," alisema Mpogoro.

Alisema kilimo ni jadi ya wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ukiwamo Mkoa wa Mbeya kwa maelezo kuwa wananchi wanajituma bila kulazimishwa hivyo akawataka wataalamu kutimiza wajibu wao.

Alisema kwa sasa serikali imeanzisha utaratibu wa kuweka ruzuku kwenye mbolea na pembejeo zingine za kilimo, hivyo akawataka wataalamu kuhakikisha wanawasaidia masuala ya utaalamu.

Mpogoro alisema serikali imewapendelea wataalamu wa kilimo nchini kwa kuwawezesha vitendea kazi (pikipiki), hivyo kazi yao ni kutumia vifaa hivyo kuwafikia wakulima kwenye mashamba yao na kuwapa elimu.

Aliwataka kuhakikisha wanazitumia pikipiki walizopatiwa kwa kazi ya kilimo na kwamba zimewekewa mifumo ambayo wakikiuka matumizi zinatoa taarifa.

# OTTU yaandaa mtaala wa kozi za muda mrefu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHUO cha Wafanyakazi Tanzania (OTTU) kilichopo jijini Mbeya, kimeanza kuandaa mtaala mpya wa masomo ambao utawafanya wafanyakazi wa kada mbalimbali kusoma kozi za muda mrefu na kuwaongezea zaidi maarifa.

Bodi ya wakurugenzi wa chuo hicho, ilikutana na wadau wa elimu kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali ya yanayohusu maendeleo ya chuo hicho ikiwamo maboresho ya mitaala inayotumika kufundishia.

Mkuu wa chuo icho, Hezron Kaaya, alisema kwa sasa wanatoa kozi za muda mfupi ambazo huwa hazizidi miezi sita jambo ambalo wamebaini kuwa linahitaji kuboreshwa ili kuwaongezea zaidi maarifa wafanyakazi.

Alisema kwa sasa wanakusudia kuanza kutoa kozi ya mwaka mmoja ambayo itawafanya wanafunzi kusoma vitu vingi zaidi na kuboresha utendaji kazi wao kwenye vituo vyao vya kazi na kuboresha tija.

"Miongoni mwa kozi ambazo tutaanza nazo ni kozi ya rasilimali watu na kozi ya uhusiano kazini ambazo kulingana na mazingira ya sasa zina uhitaji mkubwa kwa wafanyakazi, tunaamini kwamba wanafunzi wakikaa hapa mwaka mzima watakuwa wamepata maarifa muhimu," alisema Kaaya.

Mmoja wa wajumbe wa bodi ya wakurugenzi ya chuo hicho, Joseph Sayo, alisema kikao walichofanya juzi kilikuwa cha kwanza cha utendaji ambacho ndicho kinaanza mchakato wa maboresho. Alisema katika kikao hicho walijadiliana mambo mbalimbali ikiwamo uboreshaji huo wa mitaala ili kuendana na mazingira ya sasa pamoja na mahitaji ya wanafunzi ambao wanasoma chuoni hapo.

Alisema baada ya kukamilisha mchakato huo watauwasilisha katika Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa ajili ya kusajiliwa ili uendelee kutumika chuoni hapo.

Mwenyekiti wa bodi ya chuo hicho, Tamimu Salehe, alisema kozi zinazotakiwa kutolewa chuoni hapo zina mahitaji makubwa kazini na hivyo watahakikisha wanafanikisha kusajili na kuanza kuzifundisha.

"Lakini ni lazima kuhakikisha kwamba wanafunzi wanasoma katika mazingira ambayo ni mazuri na rafiki, kwa hiyo hayo yote tunayaboresha kupitia vikao vyetu tunavyoendelea navyo hapa," alisema Tamimu.

Mwakilishi wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Mahija Waziri, aliutaka uongozi wa chuo hicho kuandaa mtaala ambao unaendana na vigezo vilivyowekwa na baraza hilo.

Alisema moja ya vigezo hivyo ni kuhakikisha kozi hizo zinaendana na mahitaji ya soko la ajira pamoja na kufanya utafiti mbalimbali.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alishauri uongozi wa chuo hicho kuangalia namna ya kutoa mafunzo pia kwa wafanyakazi wa sekta zisizokuwa rasmi. Alisema kwa sasa chuo hicho kinaonekana kama ni cha wafanyakazi wa serikali pekee na hivyo kuwafanya wafanyakazi wa sekta binafsi kutokithamini.

## Rais Dk. Mwinyi: Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itaendelea kuboresha na kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, mazingira ya kufanyia kazi kwa ujenzi wa ofisi za kisasa.

Amesema pia itaendelea kuboresha upatikanaji wa vitendea kazi na utoaji wa mafunzo kwa watumishi ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo.

Aliyasema hayo jana katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Zanzibar na kuzindua mifumo mitatu ya kielektroniki.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali italinda na kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kila hali ya uchumi itakaporuhusu na kupandisha pensheni, kwamba kwa wastaafu tayari imeanza utaratibu mpya wa kulipa pensheni jamii kwa mwaka huu.

Alisema tangu Serikali ya Awamu ya Nane ilipoingia madarakani jumla ya mifumo 28 ya kielektroniki imetengenezwa kwa kuongeza ufanisi katika uwajibikaji na utoaji wa huduma bora.

"Mifumo mitatu imezinduliwa rasmi leo ikiwa ni pamoja na mfumo jumuishi wa taarifa za watumishi na malipo ambao utakuwa na mchango mkubwa wa uwekaji na uhifadhi wa taarifa za watumishi na kurahisisha mwenendo wa miamala ya fedha kwa kudhibiti wizi wa fedha za serikali," alisema.

Alisema mfumo wa ZanAjira ni muhimu katika kurahisisha shughuli mbalimbali zinazohusu ajira na kuimarisha misingi ya usawa. Aidha, Rais Dk. Mwinyi aliwataka watumishi wote kuitumia mifumo yote iliyoanzishwa ili kuleta tija iliyokusudiwa na kuimarisha ufanisi katika serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Pia aliwahimiza viongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao uongeze kasi katika kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema viongozi na watumishi wengine wana wajibu wa kuwajibika kumsaidia Rais Dk. Mwinyi ili kufikia malengo yake kwa wananchi wa Zanzibar.

Naye Waziri wa Menejimenti na Utumishi wa Umma, Joegh Simba Chawene, alisema kundi la watumishi wa umma ndio rasilimali muhimu zaidi.

Hivyo aliwaomba watumishi wenzake kuhakikisha wanawajibika ipasavyo katika kufanya kazi kwa bidii ili kuona Watanzania wanapata huduma zinazostahiki na wanaridhika na kile wanachokitaka kutoka kwao.

Alisema utumishi wa kimazoea sasa hauna nafasi na utaondoshwa kwa mifumo hiyo inayoanzishwa kwa lengo la kuhakikisha kila mtumishi anawajibika katika nafasi yake.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mansura Mosi Kassim, alisema maadhimisho hayo yanatoa fursa kwa tasisi na watumishi kujitathmini na kutafakari hatua iliyofikiwa katika kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika kutoa huduma kwa umma na kutekeleza malengo na mikakati ya serikali.

# UNDP, serikali wazindua mpango matumizi fedha ya bioanuai

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa kushirikiana na Serikali ya Zanzibar imezindua mpango wa matumizi ya fedha za bioanuai kwa ajili ya usimamizi endelevu wa bioanuai Zanzibar.

Akizindua mpango huo visiwani humo, Katibu Mkuu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajak, alisema, bioanuai za baharini na ardhini ni uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar.

Alisema pia zimesaidia upatikanaji wa ajira kwa idadi kubwa ya watu na kuongeza kwa pato la taifa kupitia sekta ya utalii na uvuvi.

"Kwa kuzingatia umuhimu wake Serikali ya Zanzibar imejumuisha masuala ya bioanuai katika mpango wa maendeleo wa mwaka 2050 ambao unalenga kuongeza maeneo ya hifadhi ya baharini pamoja na misitu ili kuhakikisha uendelevu wa kiikolojia," alisema Dk. Shajak.

Naibu Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa UNDP, Sergio Valdini, alisema shirika hilo litaendelea kujitolea kulinda thamani ya viumbe hai, kutokana na umuhimu wa ustawi na mafanikio kwa wakati huu na vizazi vya baadaye.

Aidha alisema, miongoni mwa vipaumbele vya kifedha kwa viumbe hai, kupitia mpango wa mwaka 2022/2026 shirika limepanga kutengeneza uwezo wa kitaifa na kimataifa kutokana na rasilimali za kiutandawazi, kujenga ushirikiano mzuri baina ya serikali na taasisi binafsi.

Naye Ofisa Miradi wa UNDP, Abasi Salum Kitingo, alisema mpango huo utasaidia serikali kukusanya fedha zinazohitajika katika bioanuai na kutekeleza kwa urahisi katika kufikia sera ya uchumi wa buluu.

Alisema wamefanikiwa kufanya tathmini ya sera na kuweka vipaumbele 13, ikiwamo, ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi sambamba na kuweka mazingira bora ya hali ya hewa.



Meneja Mradi wa Kampuni ya Orxy, Joseph Soka, akionyesha bomba jipya la kupokea gesi la nchi 10, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa bomba hilo, litakaloongeza upatikanaji gesi kwa wateja wa kampuni hiyo Kigamboni, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yawaondoa hofu wananchi udhibiti bidhaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shaban, amesema serikali inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini ikiwamo vyombo vya moto.

Aliyasema hayo baada ya kuweka jiwe la msingi kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto eneo la Maruhubi Zanzibar.

Alisema uwekaji wa jiwe hilo ni jambo kubwa linaloonyesha ari ya kuunga mkono kasi ya serikali katika nia yake ya kuleta mabadiliko makubwa na maendeleo katika sekta za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Aidha, alisema wizara katika nia yake ya kusimamia mipango ya taasisi zake kulinda afya na usalama wa wananchi, kuwa na mazingira endelevu ya kukuza biashara ya ushindani na kukuza viwanda vya ndani kupitia Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imewekeza katika miundombinu ya viwango.

Waziri Shaban, alisema uwekaji wa jiwe hilo pia umetimiza malengo yake ya kuwa na kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto ikiwa ni hatua ya kuimarisha taasisi hiyo ili kufanya kazi zake kitaalamu zaidi.

Alisema baada ya ZBS kuwa na sheria ya viwango ya mwaka 2011 ilifanya kazi za kuandaa viwango hivyo na kuanza kuvisimamia katika hatua nzima ya utekelezaji wa kazi zake.

Alisema taasisi hiyo ilitakiwa kwa mujibu wa sheria isimamie ubora wa bidhaa ikiwamo vyombo vya moto.

Waziri huyo alisema kwa mwaka wa fedha 2018/2019 (ZBS) iliandaa mradi wa kuanzishwa kituo kikubwa cha ukaguzi wa vyombo vya moto kitakachokuwa na vifaa vya kisasa vya kukagulia vyombo hivyo.

Waziri Shaban alisema kituo hicho pia kitaondoa changamoto ya urasimu na usumbufu katika utiaji wa huduma ya upasishaji wa vyombo vya moto kwa kuwa huduma zote muhimu zitatolewa katika eneo moja.

Aidha, alisema kituo hicho kitaongeza uwezo na ufanisi katika ukaguzi wa vyombo hivyo ambapo itapelekea kuwa na usalama wa matumizi ya vyombo hivyo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ZBS, Mwanaidi Saleh Abdalla, alisema kituo hicho kina umuhimu mkubwa katika ukaguzi wa vyombo vya moto nchini.

Aliipongeza tasisi hiyo kwa kufanya kazi kwa uadilifu na uaminifu, huku wakifuata maagizo yanayotolewa na bodi hiyo kufikia malengo ya serikali na kuanzishwa kwa tasisi hiyo muhimu nchini.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Yusuph Majid Nassor, alisema ujenzi wa kituo hicho utakamilika Agosti mwaka huu kwa ajili ya kuanza kazi.

Alifahamisha kuwa kituo hicho kinajengwa na makandarasi wa ndani ya nchi na kitakuwa na uwezo wa kuhudumia magari 150 kwa siku.

Alisema kukamilika kwa kituo hicho kitaisaidia kukagua magari kitaalamu na njia za kiteknolojia zaidi na kupunguza msongamano wa watu kusubiri kukaguliwa magari yao.

# Aitaka benki kuwezesha fursa soko huru la biashara Afrika

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

MKUU wa Wilaya ya Arusha ameitaka Benki ya Maendeleo TIB kuwawezesha wawekezaji na wafanyabiashara kunufaika na fursa za kuwapo kwa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) ili kuongeza ushiriki wa Tanzania katika soko hilo.

Felician Mtahengerwa alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa wadau wa benki hiyo Kanda ya Arusha uliofanyika katika Ukumbi Benki Kuu Tawi la Arusha.

Mkutano huo ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi kwa Umma na ulilenga kupata maoni ya wadau.

Mtahengerwa alisema Benki ya Maendeleo TIB haina budi kutekeleza kwa vitendo kaulimbiu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2023 ya 'Kufanikiwa kwa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) kunahitaji usimamizi wa utumishi wa umma wenye mtazamo wa kikanda.

"Kwa kutambua nafasi yenu kama benki ya kisera inayosaidia serikali kutekeleza mipango na sera za maendeleo kama zilivyoainishwa katika mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya taifa, Benki ya Maendeleo TIB haina budi kusaidia ushiriki wa wawekezaji wetu kwenye AfCFTA.

Aliongeza kuwa AfCFTA ina manufaa mengi kwa Tanzania ikiwamo kuongezeka kwa uzalishaji na ajira kwa wakulima na wadau wanaohusisha na mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo pamoja na upatikanaji wa soko kubwa la bidhaa na huduma lenye idadi ya watu takribani bilioni 1.2 kulinganisha na idadi ya watu takribani milioni 522 katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Afrika Kusini mwa Afrika (SADC).

Kwa mujibu wa Mkataba wa AfCFTA, nchi wanachama wanapata fursa za kuongezeka kwa tija na ubora kwa bidhaa na huduma kutokana na kuongezeka kwa ushindani na hivyo kupelekea kupungua kwa bei za bidhaa.

Kaimu Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy, alisema kaulimbiu ya Wiki ya Utumishi wa Umma inatoa fursa kwa benki hiyo katika kuchagiza shughuli za biashara na uwekezaji nchini.

Alisema Benki ya Maendeleo TIB inahakikisha inatekeleza kwa vitendo uwezeshaji wa sekta binafsi kama ilivyowekwa bayana katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 wenye lengo la kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Aliongeza kuwa benki inatumia fursa ya uimarishaji wa mifumo ya sheria na ya kitaasisi iliyofanywa na serikali hususan Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa lengo la kuboresha usimamizi na uratibu pamoja na mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu wa programu ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

"Tunaishukuru serikali kwa kuonyesha nia na utayari wa kutuongezea mtaji, hali inayotupa fursa ya kutimiza malengo makubwa zaidi. Kutokana na kuwapo mazingira haya wezeshi ya kimtaji, benki itaendelea kuchangamkia fursa za maombi ya mikopo kutoka sekta za umma na binafsi hasa ile miradi ya maendeleo inayokidhi vigezo vya njia ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuendana na ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi," alisema.

Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Afrika yaani uliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Septemba 2021.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akiongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Bank of Africa Tanzania, Adam Mihayo (wa pili kulia), wakati ujumbe wa benki hiyo ulipomtembelea ofisini kwake jijini Dodoma wakati wa kikao cha bajeti mwishoni mwa wiki. Mwingine ni Mkuu wa Kitengo cha Fedha wa Benki, Derick Lugemala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Promosheni ya Airtel yawapa neema wateja

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAKAZI saba wa Mkoa wa Dodoma wamejishindia zawadi mbalimbali kupitia promosheni ya 'Upige Mwingi na Airtel kwa kupata vifaa vya ndani ambavyo vinasaidia kubadilisha maisha yao.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya kukabidhi runinga na majokofu kwa washindi, Mkurugenzi Mkuu wa Mawasiliano wa Airtel Tanzania, Beatrice Singano, alisema shindano hilo ni la kipekee kwa kuwa kila mteja au wakala anaweza kuwa mshindi. Wametengewa Sh. milioni 250 kwa ajili ya promosheni hiyo.

"Wateja na mawakala wanaweza kujishindia zawadi za hapo kwa papo kama vile muda wa maongezi, pikipiki, jokofu, fedha taslimu kuanzia milioni moja mpaka milioni 50 kila siku. "Mbali na zawadi hizo, Airtel pia imeongeza sababu nyingine ya kutabasamu kwa wateja wetu kwani sasa wateja wote wa Airtel wanaweza kuangalia salio la akaunti za Airtel Money bila makato," alisema Singano.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkuu wa Mauzo wa Airtel mkoani hapa, Salum Ngululu alisema: "Mpaka mwisho wa promosheni hii jumla ya washindi 90 watajishindia zawadi ya Sh. milioni moja, washindi 48 wa majokofu ya milango miwili kila wiki, televisheni ya inchi 55, washindi wawili wa pikipiki katika droo ya mwezi na mwisho mteja wetu mmoja ataibuka na shangwe la zawadi ya Sh. milioni 50.

"Airtel inaendelea kuupiga mwingi pamoja na wateja wake ikiwa imesambaza huduma zake kote nchini na kufungua maduka maalum ya Airtel Money zaidi ya 3,500 na wakala zaidi ya 2,000 huku ikiendelea kuwekeza katika kupanua mtandao wa 4G kwa minara yake yote na kuwafikia Watanzania wote hasa wanaoishi maeneo ya vijijini," alisema Ngululu.

Akipokea zawadi yake ya televisioni, Mkazi wa Dodoma, Thabiti Hemedi, aliishukuru Airtel kwa zawadi hiyo japo hakuitarajia, hivyo akawataka wateja wengine 'kuupiga mwingi' ili washinde zawadi kama yake kwa kuwa zawadi zinatolewa 'bila mchongo'.

Mshindi mwingine aliyejinyakulia jokofu, Silvano Chigwaye, alisema zawadi zote zinazotolea na kampuni hiyo kupitia promosheni zake ni za kweli na hakuna upendeleo.

# Wasaka mbinu za kuimarisha huduma

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya ufundi ya serikali mtandao imefanya kikao cha kwanza kujadili namna ya utekelezaji wa majukumu yake ili kuhakikisha jitihada za serikali mtandao zinaimarika na kuleta tija kwa umma.

Kikao hicho kilifanyika juzi katika Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) jijini Dodoma, kikiongozwa na Kaimu Mwenyekiti, Eric Kitali, Mkurugenzi wa TEHAMA Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Eric alisema kamati hiyo ipo kwa mujibu wa kifungu Na. 17 cha Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019, ambapo miongoni mwa majukumu yake ni kutoa ushauri wa kitaalamu, ili kuhakikisha utekelezaji wa Serikali Mtandao unakuwa ni wenye tija na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Alisema kamati ina wajumbe wachache kulinganishwa na idadi ya wizara na taasisi za serikali na kuwasihi wajumbe kutenda haki kwa kuwajibika na kuhakikisha wanatoa ushauri wenye tija katika eneo la TEHAMA ili kuhakikisha serikali mtandao inaimarika na kuleta tija.

"Ikiwa kamati hii itafanikiwa kuifanya mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma izungumze tutakuwa tumeisaidia sana serikali, kwani itaokoa rasilimali fedha na rasilimali watu," alisisitiza.

Katibu wa Kamati hiyo, Sylvani Shayo ambaye ni Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa TEHAMA e-GA alimtaja baadhi ya majukumu ya kamati hiyo kwa mujibu wa kifungu Na. 17(4) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019.

Majukumu hayo aliyataja kuwa ni; kupitia na kutoa mapendekezo juu ya Sera ya Serikali Mtandao itakayotekelezwa katika taasisi za umma, kupitia na kutoa mapendekezo juu mpango mkuu wa serikali mtandao na mkakati wake utakaotekelezwa na taasisi zote za umma.

"Kamati pia kupitia na kutoa mapendekezo juu ya miradi na programu za kitaifa za serikali mtandao na kutoa miongozo ya kiufundi katika kutatua migogoro kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya TEHAMA katika taasisi za umma," alisema.

Majukumu mengine aliyataja ni kuishauri kamati ya kitaifa ya serikali mtandao kuhusu masuala ya serikali mtandao, kuandaa ripoti za robo mwaka na kuziwasilisha katika kamati hiyo.

Kamati hiyo iliazimia kuweka mikakati ya kupunguza udurusu wa mifumo na kuhakikisha mifumo yote ya TEHAMA, katika taasisi za umma inawasiliana na kubadilishana taarifa kupitia Mfumo Mkuu wa ubadilishanaji taarifa serikalini (GoVESB).

Kamati hiyo pia ilimchagua Connie Francis Mkurugenzi wa TEHAMA Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuwa Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo.

# Zelensky: Udhaifu wa Russia umedhihirika

**KIEV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, ameeleza kwamba uasi wa kundi la Wagner walioufanya nchini Russia, unaonyesha udhaifu wa jumla wa taifa hilo ambao ni mahasimu wake.

Ikiwa ni kauli yake ya kwanza juu ya matukio ya Russia, Rais Zelensky, alieleza kuwa yeyote anayechagua njia ya uovu anajiangamiza mwenyewe.

"Rais wa Russia, Vladimir Putin, anatuma mamia ya maelfu ya watu vitani ili kujizuia katika mkoa wa Moscow ili kujilinda dhidi ya wale ambao yeye mwenyewe amewapa silaha," alisema.

Kiongozi wa Kanisa la Othodoksi nchini Urusi na mshirika wa Rais Putin, alisema jaribio lolote la kuanzisha mifarakano nchini Russia ni uhalifu mkubwa ambao hauwezi kuungwa mkono wala kutoa nafasi ya kujitetea.

"Ninatoa wito kwa wale waliochukua silaha kuwaelekeza dhidi ya ndugu zao kufikiria upya chaguo lao juu ya kuunga mkono juhudi za Putin na kuzuia machafuko nchini Russia," alisema.

Katika ukurasa wake wa Twitter, Rais wa Baraza la Ulaya, Charles Michel, alisema anafuatilia kwa karibu hali ya Russia na kuwasiliana na viongozi wa Ulaya na washirika wa G7, baada ya kundi la Wagner kuingia katika uasi.

"Hili ni tatizo la ndani ya Russia, usaidizi wetu kwa Ukraine na Volodymyr Zelensky hautetereki," alisema.

Katika mahojiano na BBC, mkuu wa serikali ya Uingereza, Rishi Sunak, alitoa wito kwa wahusika wote kuwajibika na kulinda wananchi kwa kile kilichotokea Russia.

Naye Rais wa Baraza la Italia Giorgia Meloni, alieleza kuwa matukio hayo yanaonyesha jinsi uchokozi dhidi ya Ukraine pia unavyosababisha kukosekana kwa utulivu nchini Russia, huku Waziri wake wa Mambo ya Nje, Antonio Tajani, akitoa wito kwa raia wa Italia walioko Russia kuwa makini.

**RFI**




Mkuu wa kundi la Wagner, Yevgeny Prigozhin, akitembea kwa kujihami katika mitaa ya Rostov-on-Don Russia. **PICHA: REUTERS**

## Wagner yasitisha uasi kuepusha umwagaji damu

**MOSCOW, Russia**

KIONGOZI wa mamluki wa Wagner, Yevgeny Prigozhin, ametuma ujumbe kwenye kituo chake cha Telegram akisema amekubali kusimamisha harakati za wanajeshi wake wanaosonga mbele kuelekea mji mkuu wa Russia.

Kituo cha habari cha Rossiya 24 kilisema jana kuwa kiongozi huyo wa Wagner Prigozhin, alitoa kauli hiyo baada ya kufanya mazungumzo na Rais wa Belarus, Alexander Lukashenko.

"Prigozhin alikubali pendekezo la Lukashenko la kusimamisha harakati za Wagner katika eneo la Russia na kwa hatua zaidi za kupunguza mvutano," ilisema, ikinukuu vyombo vya habari ya Lukashenko.

Pia ilisema ilikuwa inathibitisha kwamba inawezekana kupata njia inayokubalika ya kupunguza hali ya taharuki kwa hakikisho la usalama kwa wapiganaji wa Wagner, na kwamba mazungumzo hayo yalikubaliwa na Rais wa Russia, Vladimir Putin.

Naye mkuu wa Wagner, Yevgeny Prigozhni, alieleza kuwa sababu ya maamuzi waliyoyafanya awali ni kutokana na kuwepo kwa hatua za kutaka kuvunja kampuni ya kijeshi ya Wagner, na kwamba walichokifanya ilikuwa ni maandamano ya haki.

"Katika saa 24, tulifika ndani ya kilomita 200 kutoka Moscow. Kwa wakati huu hatukumwaga hata tone moja la damu ya wapiganaji wetu," alisema.

"Sasa wakati umefika ambapo damu inaweza kumwagika, kuelewa wajibu kwa uwezekano kwamba damu ya Warussia itamwagika upande mmoja, tunageuza misafara yetu na kurudi kwenye kambi kama ilivyopangwa," alisema Prigozhin.

Akijibu hotuba ya Rais wa Russia, Prigozhin alithibitisha katika rekodi ya sauti kwamba mkuu wa Kremlin ana makosa makubwa kwa kuwashutumu wapiganaji wake kwa uhaini, huku akisisitiza kwamba wao ni wazalendo.

"Sisi ni wazalendo, na wanaotupinga leo ni wale waliojikusanya kuzunguka majungu," alisema.

Wakati huo huo wakuu wa mabaraza mawili ya Bunge la Russia wametoa wito wa kumuunga mkono Rais Putin.

**BBC**

## Mlipuko wa gesi China wanne wakamatwa

**YINCHUAN, China**

POLISI China wamekamata watu wanne kwa tuhuma za kuhusishwa na mlipuko uliotokea juzi kwenye mgahawa ulioko katika mji wa Yinchuan kaskazini magharibi mwa nchi hiyo na kusababisha watu 31 kuuawa.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya serikali, mlipuko huo wa gesi ulipotokea katika mgahawa wa kuchoma nyama Jumamosi pia ulijeruhi watu saba.

Ilielezwa kuwa tukio hilo lilifanyika katika mkesha wa mapumziko ya siku tatu ya tamasha la mashua ya Dragon wakati watu wengi nchini China walienda nje na kujumuika na marafiki.

Shirika la habari la serikali la Xinhua, lilibainisha kuwa washukiwa hao ni pamoja na mmiliki wa mgahawa, wanahisa wawili na meneja.

Pia ilielezwa kuwa walikamatwa kwa madai ya kusababisha ajali mbaya kwa uzembe na kwamba uchunguzi wa uhalifu huo unaendelea.

Xinhua ilisema ofisi ya usalama wa umma ya eneo hilo ilikuwa imezuia mali za watu tisa, wakiwamo wanne waliokamatwa.

**VOA**

## UN yataka Darfur kuangaliwa kurejesha amani

**DARFUR, Sudan**

UMOJA wa Mataifa (UN), umetoa wito wa kuchukuliwa hatua za haraka kukomesha mauaji ya kiholela ya watu wanaokimbia El Geneina mji mkuu wa jimbo la Darfur Magharibi.

Kwa zaidi ya miezi miwili, jeshi la Sudan linaloongozwa na Abdel Al-Burhan limekuwa katika mapigano na kikosi cha dharura cha (RSF) kinachoongozwa na naibu wake wa zamani, Mohamed Daglo.

Ilielezwa kuwa ghasia mbaya zaidi zimetokea Darfur, jimbo kubwa la magharibi kwenye mpaka na Chad, jambo lililo usukuma Umoja wa Mataifa kuonya kuwa mzozo huo umechukua mwelekeo wa vita vya kikabila.

Msemaji wa ofisi ya haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa, Ravina Shamdasani, alisema wana wasiwasi mkubwa kwamba mauaji hayo ya kiholela yanaendelea Darfur, huku wakiomba hatua za haraka zichukuliwe.

"Watu wanaokimbia El Geneina lazima wahakikishiwe kupita salama na mashirika ya kibinadamu yaruhusiwe kuingia katika eneo hilo kukusanya miili ya waliouawa," Shamdasan.

**VOA**

# KIKWETE AWAITA IKANGAA, BAYI KUIBUA VIPAJI RIADHA

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, amewataka wanariadha wa zamani kushirikiana na Shirikisho la Riadha nchini (RT), kuhakikisha wanafufua mchezo huo ambao unaonekana kudorola ilhali umeliletea sifa kubwa taifa kwenye medani za kimataifa.

Kikwete aliyasema hayo jana wakati wa mashindano ya riadha ya JKT Marathon yaliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri kwa washiriki kukimbia mbio za Kilomita tano,10 na 21.1 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa.

Alisema mchezo wa riadha ndio wa kwanza nchini ambao umeiletea sifa Tanzania kwa kutoa wachezaji waliofanya vizuri kitaifa na kimataifa na kupata medali za mashindano mbalimbali ikiwamo kuvunja rekodi ambazo hadi leo bado zinakumbukwa.

Akitolea mfano wanariadha wa zamani waliolipa sifa taifa, aliwataja kuwa ni pamoja na Filbert Bayi, Juma Ikangaa na Mgaya Nyambui, ambao hadi leo ukitaja majina hayo kimataifa yanajulikana, hivyo wanapaswa kuwapa mbinu wanariadha wa kizazi hiki ili Tanzania izidi kung'ara kwenye michezo kimataifa.

Kikwete alisema cha kushangaza hivi sasa mchezo huo umedorora na wachezaji wamekuwa kama yatima, tofauti na soka ambapo kila iitwapo leo linazidi kusonga mbele, jambo ambalo ametaka kuwekwa mikakati kuhakikisha riadha inapaa kimataifa.

"Wanariadha wa zamani 'weekend' (mwishoni mwa juma), wekeni mikakati ya kukutana na RT ili kuhakikisha riadha inapaa kimataifa badala ya kudorora kama mchezo mgeni wakati ulishaleta medali nyingi kimataifa," alisema Kikwete.

Alisema wanariadha hao pamoja na RT, wanapaswa kutafuta wafadhili ambao watawasaidia fedha ili kuibua wanariadha chipukizi ambao watakuwa wakina Filbert Bayi wa baadaye.

Kwa upande wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini, Jenerali Jacob Mkunda, alisema jeshi hilo limekuwa likiinua vipaji vya wanamichezo na kuwawezesha kushiriki katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi.

"Jeshi hili litaendelea kuthamini, kuibua vipaji na kuendeleza michezo kwa manufaa ya Jeshi na nchi kwa ujumla, nawashukuru washiriki wa JKT Marathon mmekuwa chachu ya kufanikisha mashindano hayo, mimi na mgeni rasmi tumeshiriki Kilometa tano," alisema Jenerali Mkunda.

Naye Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Inocent Bashungwa, ameishukuru serikali kutokana na dhamira yake ya kuendeleza michezo nchini ambayo imezaa matunda ikiwamo mafanikio yanayopatikana katika timu za michezo za majeshi hapa nchini.

Washindi wa mashindano hayo kwa upande wa wanawake waliokimbia Km. 10, nafasi ya kwanza ni Nathalie Elsante ambaye alikimbia kwa dk. 34:59:5, na kukabidhiwa zawadi ya Sh. milioni moja pamoja na medali, huku mshindi wa pili akiwa ni Transford Mussa aliyeibuka na Sh. 500,000 na medali wakati wa tatu akiwa ni Anastazia Delimungo aliyeambulia medali na Sh. 300,000.

Katika mbio za Km. 10, wanaume, mshindi wa kwanza hadi wa tatu Josephate Gisemo aliyetumia dakika 29:34:47, huku pili Deuta Tesfuly akitumia dk. 29:36:50 na tatu John Nahai, nao walizawadiwa zawadi sawa na walizopewa wanawake.

Kwa upande wa Km. 21, wanawake mshindi wa kwanza ni Magdalena Shauri aliyetumia saa1:11:22, na kupata Sh. milioni 1.5 na medali, akifuatiwa na Failuna Matlaga aliyetumia saa 1:14:04 ambapo alipata Sh. milioni moja na medali na watatu ni Maselina Issa aliyetumia saa 1:16:41 na kuzawadiwa Sh. 600,000 na medali.

Mbio za Km. 21 kwa upande ya wanaume mshindi wa kwanza alikuwa Faraja Lazaro aliyetumia saa 1:3:43 na kuzawadiwa Sh. milioni 1.5, mshindi wa pili ni Paulo Makiya aliyetumia saa 1:3:50 na kuzawadiwa fedha taslimu Sh. milioni moja na medali wakati wa tatu akiwa ni Joshua Sule aliyekimbia kwa saa 1:16:41 na kuzawadiwa Sh. 600,000 na medali, huku washiriki wa mbio za kilometa tano wote nao wakizawadiwa medali.

## Kakolanya awapa maua yao Diarra, Chama

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Beno Kalolanya, amesema kwenye Ligi Kuu Tanzania anafurahishwa mno na wachezaji wawili, kipa wa Yanga, Djigui Diarra na kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, huku akitaka wachezaji wa Kitanzania wajifunze baadhi ya vitu kutoka kwao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kakolanya ambaye amemaliza mkataba wake na Simba na sasa anatarajia kujiunga na moja kati ya timu kubwa hapa nchini kwa mujibu wake, amesema nchi yetu imebahatika kuwa na aina hiyo ya wachezaji na ni jambo jema kwa wachezaji wa Kitanzania wakaangalia baadhi ya vitu ambavyo vinaweza kuwasaidia na kuwa somo kwao.

"Wachezaji ambao ninawakubali mimi kwenye ligi ya Tanzania ni kipa Diarra, hata mimi kuna vitu najifunza kutoka kwake, anajua kuanzisha mpira, anaweza kuwatoa wachezaji wawili wasiwe kwenye mchezo na kuanza na mabeki, unajua ile inaanzia utotoni, yale ni mafunzo kabisa, wenzetu wamepata bahati hiyo.

"Makipa wengi Tanzania tunajua kudaka tu, lakini tunakosa baadhi ya vitu kama vile kwa sababu hatukupata mafunzo sahihi ya ukipa tangu tukiwa wadogo, tukiona vitu kama vile inatakiwa tuvichukue, mimi kuna vitu nimechukua kutoka kwake," alisema kipa huyo wa zamani wa Prisons na Yanga.

Alisema mchezaji mwingine ni Chama, aliyemtaja ni mmoja ya wachezaji wa kiwango cha hali ya juu Afrika anayecheza Ligi ya Tanzania.

"Nchi imebahatika kuwa na wachezaji kama Chama na ligi yetu pia imepata bahati hiyo, kwa wachezaji vijana wasiache fursa ya kujifunza kutoka kwake, ni wa aina yake, namkubali sana," alisema.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, akiwa na wachezaji wa New Generation iliyoibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Green Queen, katika bonanza la michezo maalumu lililoandaliwa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Amani na kufanyika viwanja vya kwa Wazee Sebleni, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar jana. **PICHA: IKULUA**

## Kocha Mashujaa na usajili Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mashujaa FC iliyopanda Ligi Kuu juzi, Meja Mstaafu, Abdul Mingange, amesema atatayarisha ripoti ya utawala na kiufundi kwenda kwa wakuu wake kwa ajili ya kukiboresha kikosi ili kiwe imara kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Akizungumza baada ya timu yake kuichapa Mbeya City bao 1-0 juzi, mechi ikipigwa Uwanja wa Sokoine Mbeya na kupanda Ligi Kuu kwa jumla ya mabao 4-1, Mingange alisema wanajua sasa wanakwenda kwenye ligi ambayo ni ngumu, hivyo inabidi wajipange kwa kila kitu, ikiwamo kuongeza baadhi ya wachezaji wenye viwango na wazoefu.

"Tunashukuru Mungu kwa kupanda daraja, hizi ni juhudi za Mkuu wa Majeshi aliunda kamati ya kuisaidia timu, wachezaji tuliwaongezwa posho, pia mkuu wa mkoa na wa wilaya ambao walihamasisha sana wananchi kuiunga mkono timu na ndiyo maana unaona walijaa sana siku ile pale Lake Tanganyika na hata hapa Mbeya, nusu nzima ya mashabiki wametoka Kigoma, hawa wote wamefanya kazi yangu kuwa nyepesi kidogo," alisema kocha huyo.

Akizungumzia maandalizi ya kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu 2023/24, alisema atatayarisha ripoti ambayo itakuwa ni kama dira ya kuelekea msimu ujao, ukiwamo usajili.

## Ligi Mpira Wavu kuanza leo Dar

**Na Shufaa Lyimo**

LIGI ya Taifa ya Mpira wa Wavu inatarajiwa kuanza kutimua vumbi leo, Jumatatu kwenye Uwanja wa TTC Changombe, Dar es Salaam, lengo likiwa nikupata timu za taifa zitakazoshiriki mashindano ya Afrika Agosti mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Chama cha Wavu Tanzania (Tava), Magoti Mtani, alisema ligi hiyo itashirikisha timu 22 za Wanaume na Wanawake kutoka Tanzania Bara pamoja na Visiwani ambapo 12 ni wanaume 10 za wanawake.

"Ligi hii itatusaidia kupata timu za taifa ambazo zitashiriki mashindano ya kimataifa Agosti mwaka huu, wanaume watakwenda nchini Misri na wanawake watakwenda Cameroon," alisema Mtani.

Wakati huo huo, amemtangaza Alfred Serengia kuwa Kocha Mkuu wa Timu za Taifa za Wavu kwa mkataba wa mwaka mmoja na kudai kuwa ujio wake utaongeza ushindani kwenye timu hizo kutokana na uzoefu alionao.

"Kocha tuliyemtangaza ana uzoefu wa muda mrefu, tunaamini atatusaidia kuhakikisha timu zetu zinaimarika vile vile zitakwenda kuiwakilisha vema Tanzania kwenye mashindano ya kimataifa," alisema Mwenyekiti huyo.

## ZISIKUPITE

### HAKIMI ATAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City inafikiria kuwasilisha ombi la kumnunua beki wa kulia wa Paris St-Germain, Achraf Hakimi, mwenye umri wa miaka 24 na "haitasita" kulipa ada kubwa kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco. **(Marca)**

### UNITED NA WACHEZAJI

KLABU ya Manchester United inaangalia uwezekano wa kumsajili mchezaji mwingine wa safu ya kati, huku mchezaji wa Kimataifa wa Ecuador na Brighton & Hove Albion, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21, akiongoza orodha yao, baada ya kushindwa kupiga hatua katika majaribio yao ya kumsajili Mason Mount. **(Sunday)**

### MAN UNITED NA MOUNT

MANCHESTER United haijaifurahia Chelsea baada ya habari za ofa zao kushindwa kumnunua kiungo wa kati wa England, Mason Mount, mwenye umri wa miaka 24. **(Manchester Evening News)**

### OSIMHEN AWANIWA LIVER

LIVERPOOL, Manchester United na Chelsea zitafanya mikutano na mawakala wa mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24, wiki ijayo kuhusu uwezekano wa kuhamia Ligi Kuu England. **(Express)**

### JONG ATAKIWA BAYERN

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, ameiomba klabu hiyo kumnunua kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 26, baada ya kujiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili, Declan Rice, mwenye miaka 24 kutoka West Ham. **(Foot Mercato)**

### NKETIAH AFUATILIWA

KLABU za Ligi Kuu England zinamfuatilia mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah, mwenye umri wa miaka 24, huku 'Washikabunduki' hao wakikaribia kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 24. **(Mirror)**

### KUDUS ATAJWA BRIGHTON

KLABU ya Brighton imemtambua mshambuliaji wa Ajax, Mohammed Kudus, mwenye umri wa miaka 22, kama mlengwa wao mkuu msimu huu baada ya Mghana huyo kukataa mkataba mpya katika klabu hiyo ya Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie. **(Mail)**

### HANCKO ATAKIWA NEWCASTLE

KIUNGO wa kati wa Feyenoord kutoka Slovakia, David Hancko, mwenye umri wa miaka 25, ameivutia Newcastle United ambayo inataka kuimarisha safu yao ya ulinzi. **(Mail)**

### ODOI NA CHELSEA

MCHEZAJI Callum Hudson-Odoi yuko tayari kwa mazungumzo na Chelsea, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu England zikimfuatilia winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 22. **(Express)**

### GNONTO ATAKIWA EVERTON

EVERTON ina nia ya kumleta winga wa Leeds United raia wa Italia, Wilfried Gnonto, mwenye umri wa miaka 19, pale Goodison Park msimu huu wa majira ya joto. **(Football Italia)**

### SPURS YAMTAKA VEN

KLABU ya Tottenham Hotspur imemtaja mlinzi wa Wolfsburg, Micky van de Ven, mwenye umri wa miaka 22, kwenye orodha ya wachezaji wanaowania nafasi ya ulinzi ambayo pia inamjumuisha beki wa kati wa Bayer Leverkusen na raia wa Burkino Faso, Edmond Taspoba, 24. **(Mail)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# CHELSEA SASA YAKATAA OFA YA TATU KWA MOUNT

●●●Yasisitiza kwa United kuwa tayari ilishapunguza kwa kiasi kikubwa thamani yao ya awali ya pauni milioni 70, hivyo...

**MANCHESTER, England**

CHELSEA wamekataa ombi la hivi punde la Manchester United kwa Mason Mount, lakini wametoa mazungumzo ya ana kwa ana katika juhudi za kupata makubaliano hayo, vyanzo vimeiambia ESPN.

Man United ilitoa ofa ya pauni milioni 55 pamoja na nyongeza Ijumaa, ambayo ilipigwa chini na Chelsea.

Ilikuwa ombi lao la tatu kukataliwa baada ya ofa za awali za pauni milioni 40 na pauni milioni 50.

Chelsea, kulingana na vyanzo, wamewapa United dili la paunii milioni 58 pamoja na pauni milioni saba kama bonasi zinazohusiana na kiwango cha mchezaji.

Pia, wamejitolea kukutana na maofisa wa Man United ana kwa ana kwa matumaini ya kusuluhisha hali hiyo.

Mount mwenye umri wa miaka 24, ana nia ya kuhamia Old Trafford baada ya kuondoa uwezekano wa kusaini mkataba mpya kule Stamford Bridge.

Amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Chelsea hawataki kumpoteza bure msimu ujao wa majira ya joto.

United wanaamini kwamba ofa yao ya hivi punde inaonesha mpango mzuri kwa Chelsea kutokana na Mount kuwa na mkataba wa mwaka mwingine pekee na ameiambia klabu hiyo kuwa anataka kuhama.

Hata hivyo, Chelsea wamesisitiza kwamba tayari wamepunguza kwa kiasi kikubwa thamani yao ya awali ya pauni milioni 70.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Man United wanataka kumsajili Mount haraka ili kuhakikisha mchezaji huyo wa Kimataifa wa England yuko kwenye ziara yake ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani, itakayoanza New York Julai 20, mwaka huu.

# MAN CITY YAPAMBANA KUMSAJILI GVARDIOL



**MANCHESTER, England**

MLINZI wa RB Leipzig, Josko Gvardiol, analengwa na Manchester City iwapo Aymeric Laporte ataondoka msimu huu wa majira ya joto, kwa mujibu wa ESPN.

Gvardiol yuko kwenye orodha fupi ya wachezaji wa kuchukua nafasi ya Laporte, ambaye yuko tayari kuondoka pale kwenye dimba la Etihad.

RB Leipzig tayari imempoteza Christopher Nkunku aliyetua Chelsea na Konrad Laimer kwenda Bayern Munich msimu huu wa majira ya joto na ingependelea kumbakiza Gvardiol kwa angalau mwaka mmoja zaidi.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba RB Leipzig inaweza kuomba ada ya uhamisho ya juu kama euro milioni 100 kwa sababu Gvardiol mwenye umri wa miaka 21, alisaini mkataba mpya Septemba 2022 na yuko chini ya mkataba hadi 2027.

Laporte anatathmini chaguzi zake kabla ya uwezekano wa kuondoka City na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alikosa namba mbele ya Ruben Dias, John Stones, Manuel Akanji na Nathan Ake msimu uliopita na alicheza mechi 12 pekee kwenye Ligi Kuu England.

Laporte ana mkataba pale Etihad hadi 2025 na City wataomba ada kubwa kabla ya kumruhusu kuondoka.

Wakati huo huo, vyanzo viliiambia ESPN kwamba kiungo wa kati wa City, Bernardo Silva ana ofa kutoka kwa klabu ya Saudi Arabia, Al Hilal.

# Hakimi atajwa kurejea tena Real Madrid

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid imehusishwa na mabeki wapya wa pembeni kutokana na uhaba wao wa sasa katika maeneo hayo, huku mhitimu wa akademi yao Achraf Hakimi akihusishwa kurejea Santiago Bernabeu kutoka PSG.

Wakala wa Hakimi amekiri kuwa beki huyo wa kulia ana nia ya kurejea Real Madrid msimu huu wa majira ya joto.

Ingawa ni mchezaji wa Kimataifa wa Morocco, Hakimi alizaliwa na kukulia Madrid, akitokea katika safu ya vijana kule 'Los Blancos' na kucheza mara 17 kwenye kikosi cha kwanza.

Hakimi alijiunga na Borussia Dortmund kwa mkopo wa miaka miwili mwaka 2018 kabla ya kusaini Inter Milan kwa uhamisho wa kudumu.

Alijidhihirisha kuwa mmoja wa mabeki wa pembeni bora zaidi duniani, lakini akaondoka kwenda Paris Saint-Germain baada ya msimu mmoja tu pale San Siro kutokana na masuala ya kifedha ya 'Nerazzurri'.

Akiwa PSG, Hakimi ameendelea kupaa na ni eneo la uwanja ambalo Real Madrid wamehangaika kulijaza katika misimu ya hivi karibuni.

Katika mahojiano na AS, wakala wa Hakimi, Alejandro Camano, alifungua mlango wa kurejea Santiago Bernabeu.




"Achraf amekuwa mbali na Real Madrid kwa miaka mitano, lakini huwa ni nyumbani kwake, mahali fulani moyoni mwake klabu iko pale," alisema Camano.

"Kama Real Madrid wanataka kumsajili tutasikiliza, ukimuuliza utaona ni shabiki wa Real Madrid, lakini mradi wetu sasa ni wa PSG.

"Wachezaji wakuu siku zote wanaona Real Madrid kama shabaha. Ni wachezaji wangapi wangependa kwenda huko? Achraf aliishi hivyo, na ameundwa kwa maadili ya klabu."

# Azpilicueta akaribia kutua Inter

**MILAN, Italia**

CESAR Azpilicueta amekubaliana maslahi binafsi na Inter Milan na beki huyo wa Chelsea anakaribia kuhamia klabu ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Mchezaji huyo anayependwa na mashabiki wengi amekuwa hana namba mbele ya Reece James na alikaribia kuondoka Chelsea mwaka jana huku Barcelona ikihusishwa na kutaka kumsajili.

Huku usajili wa Januari, Malo Gusto, akitarajiwa kuwasili Stamford Bridge msimu huu wa majira ya joto ili kutoa ushindani zaidi kwa James, Azpilicueta ameambiwa yuko huru kuondoka Chelsea na vyanzo vimethibitisha kwa dakika 90min kwamba anakaribia kuhamia Inter.

Azpilicueta mwenye umri wa miaka 33, amezungumza na Bayern Munich na pia akapokea ofa kutoka Saudi Arabia, lakini anatazamiwa kupeleka kipaji chake Inter Milan na anatajwa kupewa miaka miwili.


Licha ya kuwa bado ana mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Chelsea, Azpilicueta anatarajiwa kuruhusiwa kuhama kama ishara ya heshima kwa miaka 11 ya utumishi wake.

Azpilicueta alijiunga na Chelsea kutoka Marseille mwaka 2012, lakini hivi karibuni alijiimarisha kama sehemu muhimu ya safu ya ulinzi ya Chelsea, akicheza kulia na kushoto na hata kubadilika kuwa beki wa kati baadaye katika maisha yake ya soka.

Kwa jumla, Azpilicueta amecheza mechi 508 Chelsea, na kumfanya awe nafasi ya sita kwenye orodha ya wachezaji bora wa muda wote wa klabu hiyo.

Chelsea na Inter wamekuwa kwenye mazungumzo katika msimu mzima wa majira ya joto kuhusu masuala mbalimbali.

Wakati 'The Blues' wameachana na mpango wa kumnunua mlinda mlango Andre Onana, mazungumzo bado yanaendelea kuhusu mshambuliaji Romelu Lukaku.



HABARI MICHEZO

# TSHABALALA ASHUSHA PRESHA SIMBA, ASEMA YUPO SANA

**Na Saada Akida**

BEKI wa Simba, Mohammed Hussein 'Tshabalala', ameshusha presha ya mashabiki wa timu hiyo kuhusu kuendelea kusalia ndani ya klabu hiyo kuelekea msimu ujao wa 2023/24.

Tshabalala amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake ndani ya Simba, huku akihusishwa kutakiwa na Klabu ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini ambayo ofa yao iko mezani kwa ajili ya kuhitaji huduma ya beki huyo wa Timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars'.

Akizungumza na Nipashe jana, Tshabalala, alisema bado yupo sana ndani ya klabu hiyo na ataendelea kuitumikia kwa msimu ujao ili kufikia malengo yao ya kurejesha mataji yote waliyoyapoteza misimu miwili iliyopita.

Alisema anaimani kubwa na viongozi wa klabu hiyo kufanya maboresho mazuri baada ya baadhi ya wachezaji kupewa mkono wa kwa heri na kwamba anatarajia kuwapo kwa maboresho makubwa kwa nyota watakaochukuwa nafasi zao.

"Kuhusu ofa ya Kaizer Chiefs kwa sasa ni mapema kuzungumzia hilo, kwa sababu sijapata taarifa rasmi ambayo inaeleza kutaka huduma yangu, kama hilo lipo basi ninaimani ikifika muda wake litakuwa wazi," alisema Tshabalala.

Aliongeza kuwa anaimani kwa maboresho yanayofanywa na viongozi wao yatakuwa na tija kwa kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao wa mashindano na hasa ukizingatia Simba wanashiriki michuano mikubwa ya Super League.

Tshabalala alisema kuondolewa kwa baadhi ya wachezaji wenzao akiwamo Jonas Mkude na Erasto Nyoni, si kwa sababu hawajui bali ni kutokana na mipango ya benchi la ufundi kuona wameshindwa kwenda na falsafa zao.

Simba hivi karibuni imetangaza kuachana na baadhi ya wachezaji akiwamo Beno Kakolanya, Mkude, Gadiel Michael, Nyoni, Nelson Okwa, Augustine Okrah, Mohamed Ouattara na Victor Akpan.



Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Mrisho Kikwete (katikati), akiwa pamoja na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson (kushoto) na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Inocent Bashungwa (kulia), katika mashindano ya riadha ya kilometa tano ya JKT Marathon, yaliyofanyika jana Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Gamondi atabiriwa makubwa Yanga

**Na Saada Akida**

KAIMU Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayay, ameangalia wasifu wa Kocha mpya wa Yanga, Miguel Angel Gamondi, na kusema hatakuwa na kazi kubwa kwa kuwa kikosi cha timu hiyo kimemaliza msimu wa 2023/24 kwa kufanya vizuri mashindano ya ndani na kimataifa.

Mayay ametoa kauli hiyo baada ya Yanga juzi kumtambulisha rasmi kocha wao mpya, Gamondi, kuja nchini kuchukuwa nafasi ya Nasreddine Nabi, ambaye ameachana rasmi na Yanga baada ya kupata ofa Klabu ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Akizungumza na Nipashe jana, Mayay alisema wasifu aliokuwa nao kocha huyo wa Yanga unathibitisha kuwa na kiwango cha ubora wa kimataifa ambao unaweza kuipeleka Yanga katika mafanikio yanayotarajiwa.

Alisema kila kocha anakuwa na falsafa zake na anaingia katika timu iliyotoka kufanya vizuri na kuwa na muunganiko mzuri wa wachezaji licha ya kuwapo kwa mabadiliko machache ya wachezaji wapya.

"Kocha Gamondi anatakiwa kuendeleza pale Nabi alipoishia, ni jambo zuri kocha aliyepita (Nabi), aliwapa nafasi kila mchezaji kucheza, hatakuwa na kazi kubwa licha ya baadhi ya wachezaji kutokuwapo sehemu ya kikosi, lakini asilimia kubwa watakuwa wale wale kwa hiyo hataokuwa na kazi kubwa kuendeleza mtangulizi wake alipoishia msimu uliopita," alisema Mayay.

Kaimu Mkurugenzi huyo aliwasisitizia viongozi wa klabu na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa na mikakati ya muda mrefu isiopungua miaka 10 ili kuweza kuwa na maendeleo endelevu.

"Tumeshawahi kukutana na viongozi wa hizi klabu na timu kuwaeleza jinsi ya kuhakikisha wanakuwa na mikakati endelevu isiopungua miaka saba hadi 10. Lakini tunaendelea kutoa semina za uongozi ili kuona tunafanikiwa malengo yetu ya kuendeleza michezo nchini hasa mpira wa miguu," alisema Mayay.

# Kikwete aifunda TFF kwa Mayele, Baleke

INATOKA UK. 24

wamejipanga vizuri katika michezo ndio maana wachezaji kutoka JWTZ na JKT wanafanya vizuri katika michuano mbalimbali ya michezo hapa nchini.

"Tumejipanga vizuri kwa upande wa michezo tutahakikisha timu zetu za soka, riadha na michezo mingine wanafanya vizuri," alisema Jenerali Mkunda.

Aidha, Spika wa Bunge, Tulia Akson, aliitaka timu ya Mbeya City kutokata tamaa badala yake kujipanga upya kwa ajili ya msimu ujao ili iweze kurejea Ligi Kuu Bara.

Alisema timu iliyowashusha nayo iljjipanga, hivyo nao wajipange kutafuta nafasi ya kurudi Ligi Kuu.

Naye Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu, alilipongeza jeshi hilo kutokana na maandalizi mazuri ya mashindano ya riadha ambayo yamefanyika na washindi mbalimbali kupewa zawadi za fedha taslimu na medali.



# Kocha Yanga atema cheche

INATOKA UK. 24

tangu alipoanza kuzifundisha timu hizo mwaka 2000, zikiwamo pia CR Belouizdad na USM Alger za Algeria.

Historia ya kocha huyo inaonyesha kuwa ameifundisha timu moja tu ya nchini kwao Argentina ambayo ni Racing Club de Avellaneda mwaka 1998 hadi 1999 na ilikuwa ni mara ya kwanza kwenye wasifu wake wa ukocha.

Kocha huyo mwenye uzoefu wa miaka 23 kwenye ukocha wa timu mbalimbali barani Afrika, nje ya bara hili pia amezifundisha klabu mbili za Falme za Kiarabu, ikiwamo Ittihad Kalba, Timu ya Taifa ya Burkina Faso akiwa kocha msaidizi, huku pia akizifundisha Al Ahly Tripoli ya Libya, Hassania Agadir ya nchini Morocco na Platinum Stars ya Afrika Kusini.

Michezo

Jumatatu Juni 26, 2023
Nipashe



Chelsea yakataa ofa ya tatu kwa Mount

UKURASA 21

# KIKWETE AIFUNDA TFF KWA MAYELE, BALEKE

●●●Pia aionya Mashujaa isilale Ligi Kuu, Mkuu wa Majeshi naye aahidi...

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Mrisho Kikwete, ameitaka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kushirikiana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), ili kuhakikisha wachezaji wazawa wanapata sifa kubwa kitaifa na kimataifa kama kina Fiston Mayele, Jean Baleke waliosajiliwa katika klabu za Simba na Yanga.

Kikwete alitoa kauli hiyo jana katika hafla ya utoaji zawadi kwa washindi wa mashindano ya JKT Marathon yaliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri uliopo jijini Dodoma kwa washiriki kukimbia mbio za Kilometa tano,10 na 22.1.

Kikwete alisema kilio chake kikubwa yeye pamoja na Watanzania nikuona wachezaji wazawa kutoka klabu kubwa na nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu Bara wanapata sifa kutokana na mchango wao kwenye klabu hizo.

"Naibu Waziri wa Utamaduni na Michezo, naomba fanyieni kazi suala hili la uibuaji wachezaji maarufu ili kuhakikisha wanapatikana kina Mayele wa Tanzania," alisema Kikwete.

Alifafanua zaidi kuwa timu za Tanzania Simba na Yanga zinafanya vizuri, lakini mchango mkubwa unatoka kwa wachezaji wa nje hivyo nao waweke mikakati ya kuhakikisha wachezaji wa Tanzania nao wanasikika na kusifiwa kama ilivyo kwa wachezaji wengine.

Mbali na hilo, alilitaka jeshi hilo kujipanga ikiwamo kuweka mikakati ya kuhakikisha timu ya Mashujaa iliopanda Ligi Kuu Bara inasajili vizuri kwa sababu inakwenda kukutana na vigogo wa soka hapa nchini.

Alisema Ligi Kuu Bara hivi sasa inaushindani mkubwa, hivyo timu hiyo ya Jeshi ya Mashujaa inapaswa kuwekeza kwa wachezaji pamoja na benchi la ufundi ili waweze kutoa ushindani katika ligi hiyo.

"Ligi Kuu ya Bara inaushindani mkubwa sana hivi sasa, kuna timu zimewekeza vizuri kwa wachezaji, makocha na benchi la ufundi, hivyo Mkuu wa Majeshi wekezeni kwa Mashujaa ili iweze kutoa ushindani," alisema Kikwete.

Kwa upande wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini, Jenerali Jacob Mkunda, alisema hivi sasa jeshi hilo linakwenda kuunda timu ya Ngome ambayo itakuwa ikitoa ushindani katika kila michezo inayoshiriki.

Jenerali Mkunda alisema

INAENDELEA UK. 23



Miguel Angel Gamondi

# Kocha Yanga atema cheche

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu mpya wa Yanga Miguel Angel Gamondi, ameongea kwa mara ya kwanza akisema iwapo watashirikiana vizuri kufanya kazi kwa pamoja na uongozi, basi wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wataendelea kufurahi kwani yeye ni kocha mzoefu wa soka la Kiafrika kwa zaidi ya miaka 20 sasa.

Akizungumza akiwa nchini kwao Argentina, kocha huyo aliyetangazwa rasmi juzi kwenye Mkutano Mkuu wa klabu hiyo, alisema uzoefu wake wa kuzifundisha klabu kubwa na zenye mafanikio kama Wydad Casablanca ya Morocco, Esperance ya Tunisia, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, atauhamishia Jangwani na kuifanya timu hiyo kuwa tishio si ndani ya Tanzania tu, bali hata kwenye mechi za kimataifa.

"Mambo wananchi, mimi ni kocha kutoka Argentina, nimekuwa kocha zaidi ya miaka 20 barani Afrika, nimezifundisha klabu kubwa za Esperance, Mamelodi Sundowns na nimepata mafanikio mazuri nikiwa na timu hizo, nimefurahi sana kujiunga na klabu kubwa kama Yanga na yenye historia nzuri katika soka la Tanzania na Afrika.

"Kwangu ni klabu kubwa yenye mashabiki wengi wenye upendo, ninaamini kama tutaunganisha nguvu zetu pamoja wanachama, mashabiki, viongozi na benchi la ufundi, wachezaji na wafanyakazi wengine, tutaendelea kupata mafanikio makubwa kuanzia pale tulipoishia," alisema kocha huyo.

Alisema amefurahi kujiunga na klabu hiyo kubwa na kuwataka wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa na subira kwani atawasili nchini hivi karibuni.

Wasifu unaonyesha kuwa kocha mpya wa Yanga analijua soka la Kiafrika kwani, historia yake inasema amezifundisha klabu nane za Afrika,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042